Nipashe

Ijumaa Januari 1, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580447

www.ippmedia.com

The Guardian digital

nipasheTZ

nipasheTZ

nipasheTZ

0745 700710

**SIMULIZI** mwanamke aliyekutwa akiwa amekufa shambani

UKURASA 3



**SHAHIDI** aeleza alivyokuta tukio la ajali vifo wanafunzi

UKURASA 4


MKINDO B
Shule yenye ujasiriamali unaodhibiti mazingira na kulisha wanafunzi wake

BUFE

IJUMAA JANUARI 1, 2021 Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

NARCO, kampuni kuu ya mifugo yenye mizizi tangu mwaka 1947


Hatimaye maisha mapya Waingereza, EU, kila mmoja 'kivyake' kibiashara

UKURASA 11

KUANZIA LEO

# Ukinaswa na kifungashio plastiki faini 500,000/-





UKURASA 2

# Waziri aibua ubadhirifu bil. 2/- urasimishaji ardhi

UKURASA 2

## Neema yaja matibabu ya kibingwa Muhimbili

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA YATARAJIA MAKUBWA 2021 UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

# Ukinaswa na kifungashio cha plastiki faini 500,000/-

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesema vifungashio vinavyotokana na malighafi ya plastiki na ambavyo havina nembo ya Shirika la Viwango (TBS), haviruhusiwi kutumika kuanzia leo.

Jana, Kaimu Meneja wa NEMC Kanda ya Kaskazini, Nancy Nyenga, aliiambia Nipashe kwamba, kwa kiwanda kitakachozalisha vifungashio hivyo, kitatozwa faini ya Sh. milioni 20 na isiyozidi Sh. bilioni moja au kifungo cha miaka miwili jela au adhabu zote kwa pamoja.

Kwa mujibu wa mtendaji huyo wa NEMC, vifungashio vinavyolengwa ni pamoja na vinavyotumika kufungasha ubuyu, barafu na vyote vya plastiki visivyokuwa na nembo ya TBS.

Akizungumzia marufuku hiyo, alisema vifungashio vyote vya plastiki visivyokuwa na nembo ya TBS, havitaruhusiwa kuanzia Januari Mosi mwaka huu, yaani leo, kwa kuwa serikali imeshapiga marufuku na kuelekeza vifungashio vinavyoruhusiwa.

"Sheria ya Mazingira ya Kuzuia Mifuko ya Plastiki ilianza kutumika Juni mwaka jana na serikali kupitia NEMC, ilitoa maelekezo ya vifungashio vinavyoruhusiwa kuwa ni pamoja na vile vyenye nembo za TBS kutoka viwandani.

"Lakini, kumeendelea kuwapo vifungashio vya plastiki vinavyozagaa mitaani na kuendelea kuchafua mazingira jambo ambalo siyo sahihi," alisema.

Kwa mujibu wa Nyenga, jana ndiyo ilikuwa tarehe ya mwisho kwa vifungashio hivyo na baada ya hapo sheria itaanza kufanya kazi.

Alizitaja faini kwa wazalishaji wa vifungashio hivyo pamoja na wanaoingiza kutoka nje ya nchi kuwa ni kiasi kisichopungua Sh. milioni 20 na kisichozidi Sh. bilioni moja au kifungo cha miaka miwili jela au vyote kwa pamoja.

Kiongozi huyo wa NEMC alisema wasambazaji wa vifungashio visivyo na nembo ya TBS, watatozwa faini ya isiyopungua Sh. milioni tano na isiyozidi Sh. milioni 50, huku adhabu kwa wauzaji wadogo ikiwa ni kuanzia Sh. 100,000 hadi 500,000 au kifungo kisichopungua miezi mitatu jela.

Alifafanua kuwa kwa mtu yeyote atakayeingiza bidhaa zilizopo kwenye vifungashio vya plastiki, atakuwa na wajibu wa kuhakikisha taka zitokanazo na vifungashio hivyo zinasimamiwa au kutupwa kwa mujibu wa kanuni za usimamizi wa taka ngumu za mwaka 2009.

"Mifuko yote ya plastiki kwa ajili ya kubebea bidhaa mbalimbali bila kujali unene wake, imepigwa marufuku kuingizwa nchini, kusafirishwa nje ya nchi, kuzalishwa, kuuzwa, kuhifadhiwa, kusambazwa na kutumika ndani ya Tanzania Bara," alisema.

Wajasiriamali wadogo wanaojihusisha na biashara hiyo, walalamikia katazo hilo na kuiomba serikali kuangalia namna ya kuboresha vifungashio hivyo na viwe nafuu kwa watumiaji wa mwisho.

Hosiana Joseph, mmoja wa wauzaji wa vifungashio katika Soko la Kilombero, alisema biashara hiyo imekuwa ikimwingizia kipato husussan kutoka kwa wafanyabiashara wa samaki.

"Tulizoea kujitafutia maisha kupitia vifungashio hivi, lakini tunaambiwa leo (jana) ni mwisho. Sijui tutafanya biashara gani tuweze kujipatia riziki ya kila siku na tuweze kujikimu kimaisha," alilalama.

# Jafo aonya ulaji wa fedha 'mbichi'

**Na Paul Mabeja, BAHI**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amewataka watumishi wa Halmashauri ya Bahi mkoani Ddooma, kuacha tabia ya kula fedha mbichi za mapato, huku akiwaagiza wote wenye tabia hiyo kuacha mara moja.

Pia, amezitaka halmashauri zote nchini kuangalia namna bora ya kuachana na matumizi ya karatasi na kutumia vishikwambi hususani kwa madiwani na wakuu wa idara.

Jafo alibainisha hayo jana wakati akizungumza na watumishi wa halmashauri hiyo, akisema kuna watu waliopewa dhamana, wakiwamo wenyeviti, mapato mengi hawayaingizi katika akaunti.

"Kwa hiyo, Bahi mambo mengi ni mazuri, lakini hapo tu ndiyo tatizo, wale waliopewa dhamana kukusanya pesa, kule kuna ujanja ujanja mwingi, wengine wanacheza na mashine za kukusanyia mapato (POS) wengine mtu anakuja hakatiwi risiti katika POS, mwingine anakusanya lakini pesa haiendi benki," alisema.

Jafo alisema anaamini Wilaya ya Bahi ina watendaji wengi wa aina hiyo, akiwataka watumishi hao kutambua kuwa uadilifu ni jambo la msingi.

Alibainisha kuwa, katika mambo yote, ajenda ya ukusanyaji mapato ni kipaumbele kilichowekwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa sasa.

"Mkurugenzi hili tu ndiyo linaharibu halmashauri yako na wakati mwingine hawafanyi pekee yao, watu wa vijijini wanashirikiana na watu wa makao makuu ya wilaya, hili lisimamie," aliagiza.

Waziri huyo alishauri kuwapo utaratibu mzuri wa kila halmashauri nchini kuhakikisha madiwani wanaachana na matumizi ya karatasi na badala yake watumie vishikwambi.

"Lengo ni kuondoa matumizi ya fedha nyingi za serikali na badala yake fedha hizo zielekezwe kusaidia wananchi. Niipongeze Wilaya ya Bahi kwa kuwa ya mfano, mmewanunulia madiwani wenu na wakuu wa idara vishikwambi," alisifu.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akizungumza na watendaji wa sekta ya ardhi (hawapo pichani), katika Chuo cha Ardhi Morogoro tarehe 30, Desemba 2020, wakati wa ziara ya kukagua utendaji kazi wa sekta hiyo na miradi inayoendeshwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) mkoani Morogoro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri abaini ubadhirifu bil. 2/- ardhi

**Na Munir Shemweta,** MOROGORO

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amebaini ubadhirifu wa zaidi ya Sh. bilioni mbili uliofanywa na wakufunzi wa Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO).

Kutokana na ubadhirifu huo, amemwagiza Mkuu wa Chuo hicho, Huruma Lugala, kumsimamisha kazi mara moja Mkuu wa Utawala, Michael Lori kwa tuhuma za kushirikiana na wakufunzi wawili waliofanya ubadhirifu katika kazi ya urasimishaji.

Dk. Mabula alitoa maelekezo hayo juzi mkoani hapa wakati akizungumza na watendaji wa sekta ya ardhi na uongozi wa mkoa wa Morogoro akiwa katika ziara ya siku moja kukagua utendaji kazi wa sekta hiyo na miradi inayotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).

Alisema wizara yake ilifikiri kushirikisha na kampuni binafsi katika urasimishaji ingerahisisha kupima na kumilikisha wananchi maeneo yao, lakini matokeo yake baadhi ya kampuni na watu wachache wametumia nafasi hiyo kufanya ulaghai kwa kuchukua fedha za wananchi bila kukamilisha kazi.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, mkuu wa utawala wa chuo hicho, ameonekana kushirikiana na watuhumiwa kwa namna mbalimbali na uamuzi wa kumsimamisha ni kupisha uchunguzi wa tuhuma zinazomkabili.

Awali, Lugala alimweleza Dk. Mabula kuwa wakati uongozi wa chuo ukifanya jitihada za kukiboresha chuo ikiwamo kudhibiti hujuma mbalimbali, ilibainika baadhi ya wakufunzi kujihusisha na urasimishaji katika maeneo mbalimbali kwa kutumia jina la chuo kujipatia fedha.

Alisema chuo chake baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi na kubainika udanganyifu kwa baadhi ya watumishi wake, kiliamua kuwasimamisha wakufunzi wawili kupisha uchunguzi.

Lugala aliwataja watumishi hao kuwa ni Adolf Milungala anayetuhumiwa kujipatia Sh. bilioni 1.9 na Hamis Kindemile Sh. milioni 275 fedha zilizokuwa malipo ya urasimishaji katika mitaa 43 ya Morogoro.

Alisema wakati uchunguzi ukiendelea dhidi ya watuhumiwa, Mkuu wa Utawala, Lori, amekuwa akishirikiana na watuhumiwa kukwamisha uchunguzi na hata pale alipotakiwa kujieleza kwa barua alijibu kwa dharau na kwamba hata alipoitwa na tume ya uchunguzi aligoma kwa kisingizio cha ugonjwa.

Kutokana na maelezo hayo, Dk. Mabula aliupongeza uongozi wa chuo kwa hatua ulizochukua kuwasimamisha watuhumiwa kupisha uchunguzi na kusisitiza kuwa wizara imeanza kuchukua hatua kwa kampuni zote zilizoshindwa kukamilisha urasimishaji.

"Kutokana na tukio hili, halmashauri inatakiwa kuchukua hatua za kukamilisha upimaji katika maeneo ambayo watuhumiwa walichukua fedha na nimekiagiza Chuo cha Ardhi Morogoro kuhakikisha na kinafanya upimaji katika maeneo hayo," alisema Dk. Mabula.

Alisema lengo la wizara ni kuhakikisha kila mwananchi aliyetoa pesa apimiwe na apate haki yake ya msingi ya kupatiwa hati na kusisitiza kuwa hilo ni onyo kwa kampuni zote zisizotekeleza kazi kuchukuliwa hatua na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

HABARI KITAIFA

# Neema matibabu mapya ya kibingwa Muhimbili

Na Beatrice Shayo

SERIKALI imesema Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), itaanza kupandikiza chembechembe hai kwa wagonjwa wa saratani ya damu kuanzia Machi mwaka huu.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alitangaza neema hiyo jana alipozuru katika hospitali hiyo jijini Dar es Salaam kuona hali ya utoaji wa huduma na vikwazo vinavyowakabili watendaji wake.

Alisema kuna wagonjwa wa saratani ya damu ambao wamekuwa wakisumbuka na kupelekwa nje ya nchi kwa ajili ya kupatiwa matibabu hayo, sasa watatibia nchini.

"Wameahidi kunipa andiko zima la namna walivyojipanga na tayari kuna maeneo ambayo wameshaanza kuyafanyia kazi; upandikizaji wa uroto wa mifupa na kumekuwa na wagonjwa wa saratani ya damu, inasuambua watu inabidi wapelekwe nje ya nchi wakafanyiwe vipandikizi vya chembechembe hai.

"Sasa, hapa kwetu watakuwa wanafanya hiyo kazi, wameshajiandaa, chumba wanacho, vifaa vipo na watu wameshapewa ujuzi, madakatari na waaguzi na mashine zimeshakuja," alisema.

Alisema kuna mashine moja ya mwisho ambayo itakuwa inatumika kwenda kuzalisha mahitaji ya damu kwa kuwa wagonjwa watakuwa wanapata tiba hiyo, watakuwa wanahitaji damu nyingi, hivyo ni lazima wajiimarishe katika eneo hilo.

"Mungu akisaidia shughuli hii inatakiwa kuanza Machi mwakani (mwaka huu). Hili nimelibariki, ni eneo moja ambalo lilikuwa linatusumbua," alisema.

Alisema anatambua mchango wao mkubwa katika kuboresha huduma ya afya nchini hasa kwenye daraja la ubingwa kwa kufanikiwa kuokoa gharama nyingi zilizokuwa zinatumika kupeleka wagonjwa nje ya nchi.

Gwajima alisema ilani yao inasisitiza kuimarisha huduma za kibingwa, hivyo alitaka kujua walivyojipanga kuitekeleza katika miaka mitano ijayo.

Alisema wapo wagonjwa ambao wanakwenda Nairobi na kuchangia fedha taslimu, hivyo wamekuja na huduma hiyo ili wazipate huduma hizo nchini.

"Jengo hilo ujenzi wake unaendelea vizuri, itakapofika Februari mwaka 2021, litaanza kunyanyuliwa kwenda juu, ni mengi yaliyofanyika katika uboreshaji wa huduma kwa wagonjwa," alisema.

Alisema wagonjwa ambao wanatibiwa na hawana fedha, wanatakiwa kufuata masharti ya msamaha yaliyowekwa badala ya kuanza kulalamika.

Dk. Gwajima alisema amebaini zaidi ya Sh. milioni 800 zimetumika kutibu wagonjwa wa msamaha mwaka huu katika hospitali hiyo.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, SACP Fortunatus Musilimu, akizungumza na madereva saba kati ya 10 wa mabasi ya abiria waliokutwa na makosa mbalimbali ya usalama barabarani kabla ya kuwafikisha mahakamani jana. **PICHA: FRANK KAUNDULA**

# Akutwa akiwa amekufa shambani

Na Stevie Chindiye, TUNDURU

MKAZI wa Kijiji cha Kadewele, Fatuma Ally (46), amekutwa akiwa amefariki dunia shambani kwake katika tukio linalohusishwa na ugomvi wa mipaka ya mashamba.

Mashuhuda wa tukio hilo walisema marehemu alikumbwa na mkasa huo akiwa katika shamba la mpunga lililoko eneo la Mkatapula Mashambani katika kijiji cha Chingulungulu na mwili wake kukutwa ukiwa kwenye matope shambani hapo.

Akizungumzia tukio hilo, kaka wa marehemu, Jafari Ally, alisema dada yake aliondoka asubuhi ya Desemba 29 kwenda shambani akiwa na afya njema lakini cha kushangaza siku hiyo hakurudi bila kutoa taarifa yoyote kwa familia yake.

Alisema baada ya wanafamilia kutomwona ndugu yao, usiku wa siku hiyo, baadhi ya wanafamilia wakishirikiana na majirani, waliamka alfajiri kwa ajili ya kufuatilia nyendo zake kwa kupita maeneo mbalimbali kwa ndugu, jamaa na marafiki wakiwa wanaulizia kama ndugu yao alionekana.

Baada ya mizunguko hiyo kutozaa matunda, alisema juzi alfajiri wakiwa wamepoteza matumaini ya kumwona ndugu yao, waliamua kwenda hadi shambani ambako hakukuwa na nyumba ya kuishi na kushuhudia ndugu yao akiwa amefariki dunia na mwili wake ukiwa katika tope.

Mume wa marehemu, Kazembe Kawina, alisema amepokea kwa mshtuko taarifa za tukio hilo kwa kuwa mkewe aliondoka nyumbani kwa ajili ya kwenda kusimamia shughuli za shambani, huku yeye akibakia mjini kwa ajili ya kutafuta fedha za kuwalipa vibarua waliokuwa wakifanya kazi shambani huko.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, amethibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kwamba polisi wanaendelea na uchunguzi wa chanzo cha kifo hicho.

Pia Kamanda Maigwa aliwataka wananchi ambao wana taarifa sahihi za chanzo cha tukio hilo, kulisaidia jeshi hilo ili kuwakamata wahusika na kupisha sheria kufuata mkondo wake.

# Walalamika kutolewa katika mashamba yao

Na Mary Mosha, MOSHI

BAADHI ya wananchi wa Kata ya Kibosho Kati mkoani Kilimanjaro, wameulalamikia uongozi wa Tarafa ya Kibosho, kwa kutaka kuwaondoa kwenye shamba lao.

Wananchi hao wamedai kuwa shamba hilo walikabidhiwa na serikali baada ya kutoa maeneo yao kwa ajili ya kupisha ujenzi wa Shule ya Sekondari Kirima. Pia wamelalamikia kuharibiwa kwa mazao yao yaliyokuwa shambani.

Akizungumzia mgogoro huo, mmoja wa wananchi hao, Bonaventure Kimaro, alisema mwaka 1999 wananchi waliokuwa wakiishi karibu na shule za msingi na sekondari Kirima, shule za msingi za Masoka, Mangikida Chini, Singabora na kituo cha polisi Kirima, walitakiwa kutoa maeneo yao ili kupisha upanuzi na ujenzi wa shule hizo na serikali ilitoa ekari 37 kwa wananchi hao kama fidia.

Alisema eneo hilo lilitolewa lilikuwa na ukubwa wa ekari 154, zilizokuwa za Chama cha Ushirika cha Kilimaboro na kati ya hizo, 117 alipewa mwekezaji Vassol Agrovet, kampuni inayojihusisha na kilimo cha maua.

Hata hivyo, alisema mwaka 2005 wananchi ambao hawakufahamika, walivamia shamba hilo na kukata migomba ambayo ilikuwa shambani humo kwa madai kuwa shamba hilo limevamiwa na watu wasiojulikana.

"Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Moshi kwa wakati huo, aliingilia kati na kusuluhisha tatizo hilo, lakini mwaka 2009 watu walivamia tena mashamba hayo hali iliyosababisha kwenda mahakamani na walishinda kesi na kurudi kwenye maeneo waliyokabidhiwa na serikali," alisema.

Naye Paulo Lemence, alisema Oktoba 5, mwaka jana, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kibosho Kirima na Ofisa Tarafa ya Kibosho, walifika katika mashamba hayo na kutoa tangazo la katozo kwa wananchi kufanya shughuli yoyote katika mashamba hayo, jambo ambalo limesababisha kuwa na hofu ya hatima ya eneo hilo.

Pia alisema baada ya tangazo hilo, wakati wakitafuta suluhisho la eneo hilo, Desemba 4, mwaka jana, watendaji wa serikali walifika tena kwenye mashamba hayo, wakiwa na mwekezaji wanaliyepakana naye na walipitisha trekta na kulima mazao ya wananchi ambayo yalikuwa shambani.

Diwani wa Kata ya Kibosho Kati, Bahati Mamboma, alisema baada ya tangazo la kuzuiwa kwa wananchi kuingia katika eneo hilo, waliwataka kuwa watulivu ili kutoa nafasi kwa viongozi kulishughulikia tatizo hilo.

Evarista Kulawa, mkulima katika shamba hilo, alisema amekuwa akilima katika shamba hilo, kwa kukodishiwa na watu ambao waliojitolea kwenye maeneo yao.

Alisema kitendo hicho, kilichofanywa na mwekezaji huyo, kuharibu mazao yaliyokuwa shambani imewaumiza kwa kuwa familia zao zinategemea chakula kutoka kwenye shamba hilo.

Akijibu tuhuma za wananchi hao, Ofisa Tarafa ya Kibosho, Yusuph Munisi, alisema baada ya chama cha ushirika kutoa eneo kwa ajili ya wananchi waliotoa maeneo yao kupisha ujenzi wa shule hizo, haikufanyika hivyo na tukio hilo lilisababisha mgogoro wa muda mrefu.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kirima, alisema tangazo lilitolewa kwa wananchi kutokuingia kwenye shamba hilo, kwa lengo la kuwafahamu wahusika wanaomiliki na utaratibu walioufuata kuingia kwenye shamba hilo.

# Serikali yaanza ujenzi wa 'Day Care'

**Na Mwandishi Maalum**

SERIKALI kupitia Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Shirika la BRAC Tanzania, imeanza kuratibu uanzishwaji wa vituo vya malezi kwa watoto wadogo vitakavyomilikiwa na kuendeshwa na jamii eneo husika.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mtoto kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwajuma Magwiza, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akikagua maendeleo ya uanzishwaji wa vituo hivyo kwa manispaa za Temeke na Kigamboni, vinavyojengwa kwa ushirikiano wa wananchi, serikali na shirika hilo.

Magwiza alisema lengo la uanzishwaji wa vituo vya malezi kwa watoto katika kijamii ni kuhakikisha watoto wanapata sehemu sahihi ya kukaa na kulelewa wakati wazazi na walezi wanapokuwa katika majukumu ya kutafuta riziki.

Aliongeza kuwa vituo hivyo vya malezi pia vitasaidia kuondokana na ukatili kwa watoto wadogo ikizingatiwa kuwa hufanyiwa vitendo hivyo katika jamii wanazoishi.

"Vituo hivi vitakuwa chini ya jamii husika na vitasaidia malezi kwa watoto pale wazazi na walezi wanapokuwa katika majukumu ya utafutaji wa kipato," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Mbagala Kuu, Fabian Chilumba, alisema wameupokea mradi huo kwa dhati na atahakikisha anahamasisha wananchi kuendelea kuchangia nguvu zao kuhakikisha miradi inaisha kwa wakati na kuanza kutumika.

Diwani wa Somangila na Naibu Meya Manispaa ya Kigamboni, Steven Warioba, alisema kuna uhitaji mkubwa wa vituo hivyo katika mitaa kwa kuwa watoto wengi wanahitaji huduma ya uangalizi wakati wazazi hawapo nyumbani.

Diwani wa Kimbiji, Muhidini Budaya, alisema atashirikiana na viongozi wa Manispaa ya Kigamboni kuhamasisha wananchi kushiriki katika ujenzi wa vituo hivyo, ili kuhakikisha watoto wanapata sehemu sahihi ya kulelewa wazazi wakiwa katika majukumu ya kutafuta riziki.

Meneja Mradi wa BRAC, Novatus Tarimo, alisema shirika lao linashirikiana na wananchi katika kuhakikisha mradi wa ujenzi wa vituo hivyo kwa ngazi ya jamii unakamilika na kuanza kutumika.

Serikali kwa kushirikiana na BRAC na wananchi, kuchangia nguvu zao kuendesha ujenzi wa mradi wa vituo vya malezi kwa watoto wadogo kwenye ngazi ya jamii katika mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam. Vituo 30 vinajengwa katika mitaa ya halmashauri mbalimbali za mikoa hiyo.




Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, akifungua kikao kazi cha siku moja jana, kilichohusisha Menejimenti ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar-es-Salaam (DAWASA) na wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani, kilicholenga kuimarisha uhusiano na kutatua changamoto za upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa maeneo yao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shahidi aeleza alivyokuta miili ya wanafunzi, hali ajali eneo la tukio

**Na Jocktan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita imeanza kusikiliza shahidi wa kwanza katika kesi inayomkabili Ofisa Mpango Miji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyanghwale, Augustino Simbeye (36).

Ofisa huyo anakabiliwa na mashtaka matano ya kugonga wanafunzi wanne wa Shule ya Msingi Ibambila na kufariki dunia papo hapo, huku gari lililowagonga wanafunzi hao likidaiwa kutokuwa na bima kinyume cha Sheria ya Udhibiti wa Bima sura ya 169 mapitio ya mwaka 2002.

Mshtakiwa huyo anadaiwa kuwa Novemba 2, mwaka huu, majira ya asubuhi katika Kijiji cha Ibambila barabara ya Geita -Msalala, mkoani Geita, akiwa anaendesha gari lenye namba za usajili T 186 DPR aina ya Toyota Harrier, aliwagonga wanafunzi wanne na kufariki dunia papo hapo.

Wanafunzi anaodaiwa kuwagonga na kusababisha vifo vyao ni Shukurani Masumbuko (14) wa darasa la sita, Julius Fikineo (7) wa darasa la kwanza, Thobias Marko (19) wa darasa la tano na Kalebu Kisinza (15) wa darasa la sita.

Katika kesi hiyo inayosikilizwa mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Samuel Maweda, upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Hezron Mwasimba, ulidai kuwa una shahidi mmoja na yuko tayari kuendelea kumsikiliza shahidi huyo.

Shahidi huyo, Konstebo Issa wa Kituo cha Polisi Karumo wilayani Nyang'hwale, alidai kuwa yeye ni askari wa usalama barabarani na anakumbuka Novemba 2 akiwa kituoni hapo, alipewa taarifa na mkuu wake kuwa katika Kijiji cha Ibambila kwenye barabara ya Msalala- Geita, kuna gari lenye namba za usajili T 186 DPR aina ya Toyota Harrier limewagonga wanafunzi wanne na wamefariki dunia.

Alidai kuwa baada ya taarifa hizo alikwenda katika eneo hilo na kumkuta Mkuu wa Kituo cha Polisi Nyang'hwale, Inspekta Omari, na damu ilikuwa imetapakaa chini na miili ya marehemu ilikuwa imeshaondolewa na kupelekwa katika Kituo cha Afya Nyang'hwale.

Shahidi huyo alidai kuwa gari lililowagonga wanafunzi hao lilikuwa kilomita mbili kutoka eneo la tukio na walikagua eneo hilo wakiwa na mkulima Nyanda Rushinge ambaye alikuwa analima eneo hilo na alishuhudia ajali hiyo.

Baada ya kukagua eneo la tukio hilo, alidai kuwa hali ya hewa ilikuwa nzuri pia barabara hiyo haikuwa na kichaka chochote cha kufanya dereva asione mbali.

Alidai kuwa walichora ramani eneo la tukio pamoja na kulichukua gari hilo kwa kuvutwa hadi kituo cha polisi Karumo.

Pia alidai alibaini gari hilo lilikuwa na mwendo mkali na lilipojikita kwenye tuta liliyumba na kwenda pembeni kushoto ambako kulikuwa na wanafunzi wanne na kuwagonga wote.

Pia alidai kuwa baada ya kutoka eneo la tukio, alikwenda katika Kituo cha Afya Nyang'hwale na kukagua miili ya wanafunzi hao akiwa na ndugu wa marehemu pamoja na Dk. Samuel Kanuno.

Katika ukaguzi huo, alidai kuwa walibabini miili ya wanafunzi ilikuwa na majeraha kichwani, wengine walivunjika viuno, mikono na miguu na wote walikuwa wavulana na wanafunzi wa Shule ya Msingi Ibambila.

Shahidi huyo alidai kuwa tukio hilo lilikuwa baya sana kwa sababu lilileta taharuki kwa wananchi kwa kuwa tukio hilo haijawahi kutokea katika Wilaya ya Nyanghwale na kwamba waathirika walikuwa wanafunzi ambao walikuwa na ndoto zao na pia wazazi wao walikuwa wakiwategemea.

Baada ya shahidi kumaliza ushahidi wake, Hakimu Maweda alimpa nafasi mshtakiwa ili kumuuliza maswali na mahojiano yao yalikuwa kama ifuatavyo;-

**Mshtakiwa:** Niliendesha mwendo kasi wa namna gani?

**Shahidi:** Tairi lilionyesha jinsi ulivyokuwa na mwendo kasi. Uliwagonga wanafunzi hao wanne kwa sababu ya mwendo kasi kwa mita nane nane.

**Mshtakiwa:** Waliogongwa walikuwa mita ngapi?

**Shahidi:** Mita nane kwa kila mwanafunzi aliyegongwa.

**Mshtakiwa:** Mvua haikunyesha siku hiyo?

**Shahidi:** Mvua haikunyesha siku hiyo.

Baada ya mshtakiwa kumaliza kumuuliza maswali shahidi wa upande wa Jamhuri, Wakili wa Serikali Mwandamizi Mwasimba aliomba hapo mahakamani tarehe nyingine kwa ajili ya kuendelea kusikiliza mashahidi waliobaki.

Hakimu Maweda alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Januari 19, mwaka huu. Mshtakiwa yuko nje kwa dhamana.

HABARI KITAIFA

# Aagiza transfoma kupelekwa mgodini

**Na Dorina Makaya**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amelitaka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kupeleka transfoma mbili zenye uwezo wa MVA 2.5 na MVA 2.0 kwenye mgodi wa dhahabu unaomilikiwa kwa ushirikiano wa kampuni ya Busolwa Mining na Isinka ifikapo Januari 15.

Kalemani alitoa agizo hilo juzi, alipotembelea mgodi huo ulioko Kijiji cha Buhunda, Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza.

Alisema kupatikana kwa transfoma hizo kutawezesha kupatikana umeme wa kutosha kuendesha mitambo mgodini hapo na kupunguza zaidi ya asilimia 70 ya gharama za uzalishaji.

"Natambua kuwa tayari mgodi huu uliletewa transfoma kwa ajili ya shughuli za ujenzi, lakini ina uwezo mdogo kulingana na mahitaji na transfoma hizi kubwa mbili zilipaswa kuwa zimefika mgodini hapa mwishoni mwa Desemba, mwaka huu (mwaka jana) na ndiyo maana nimefika hapa ili kujionea hali halisi na kutoa maelekezo," alisema.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Busolwa Mining Limited, Baraka Ezekiel, alisema kuwa mradi huo ukikamilika, unatarajia kutoa ajira za kudumu kwa zaidi ya Watanzania 300 wenye taaluma mbalimbali na utakuwa chachu ya maendeleo kwa maeneo yanayozunguka mgodi, Mkoa wa Mwanza na taifa kwa ujumla.

Kutokana na maelekezo ya Waziri Kalemani, Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, aliwataka watumishi wa mgodi huo kufanya kazi kwa kasi ili kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati.



Balozi wa programu ya Uanagenzi Pacha ambaye ni mkulima wa mjini Babati, Jitu Son, akichangia mada wakati wa warsha iliyoandaliwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) kuhusu mikakati ya uzalishaji wa wataalamu sekta za kilimo, ukarimu na utalii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni tuhuma wizi vifaa vya TANESCO

**Na Elisante John,** SINGIDA

WATU tisa wanashilikiwa na polisi mkoani Singida kwa tuhuma za wizi wa vifaa mbalimbali vikiwamo vyuma vya kusukia umeme, koki, bolti na nyaya za shaba, mali ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Sweetbert Njewike, alisema thamani halisi ya vifaa hivyo bado haijafahamika huku pia akikwepa kutaja majina ya watuhumiwa kwa madai kwamba yanaweza kuharibu upelelezi wa kuwanasa watu wengine wanaojihusisha na mtandao huo.

Alisema watuhumiwa wote pamoja na vifaa vilivyokamatwa, walinaswa kutokana na msako mkali unaoendelea katika maeneo mbalimbali mkoani Singida kuanzia juzi.

Kamanda Njewike alifafanua kuwa matukio matatu kati ya manne, yalitokea siku ya juzi, yalisababisha watuhumiwa kukutwa na baadhi ya vifaa hivyo wakiwa wamevihifadhi kwenye nyumba zao katika mitaa ya Ukombozi, Minga na Ng'aida, mjini Singida.

Pia alisema watuhumiwa walikutwa na vifaa hivyo eneo la Manguamitogho, wakitorosha kutoka mradi wa umeme wa REA Sepuka kwa kutumia gari lenye namba za usajili T 446 AYC, mali ya kampuni ya Ngiheco Electrical Contractors LTD ya mkoani Arusha.

"Uchunguzi wa awali unaonyesha watuhumiwa hawa wanajihusisha na uuzaji wa vyuma chakavu. Kwa maana hiyo, wanaiba vyuma hivi muhimu kwa maendeleo ya taifa na kwenda kuviuza kama vyuma chakavu," alisema.

Kutokana na matukio hayo, Kamanda Njewike amewaomba wananchi kuendelea kushirikiana na jeshi hilo kwa kutoa taarifa pale wanapobaini dalili za uwepo wa njama za wizi wa aina yoyote ile, ikiwamo wale wanaojihusisha na wizi wa vyuma kutoka taasisi za umma.

Katika kuelekea mwisho wa mwaka na kuupokea mwaka mpya, Njewike aliwataka wakazi wa Singida kujiepusha na uhalifu wa aina mbalimbali.

Njewike aliwaonya wote watakaokaidi agizo hilo kuwa, Jeshi la Polisi halitasita kuwachukulia hatua kali, na mwisho kuwakamata na hatimaye kuwafikisha kwenye vyombo vya dola, ikiwamo mahakama.

# TAWA yatoa sababu kuua simba

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) imekemea vikali taarifa za upotoshaji zinazosambazwa kuwa imekiuka haki za wanyama kwa kumuua simba.

Pia imekemea tabia ya kuachwa wanyama wakali wakiachwa kuendelea kuleta taharuki kwa jamii na kufanya watu watatu kuuawa na tembo katika maeneo tofauti mwezi uliopita.

Ofisa Wanyamapori Mwandamizi Udhibiti wa Wanyamapori Wakali na Waharibifu kutoka TAWA, Wilbright Munuo, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari juu ya umuhimu wa kulinda wanyama sambamba na kulinda haki na uhai wa binadamu dhidi ya wanyama wakali na wasumbufu.

Munuo alisema kutokana na tabia ya wanyama wakali kuleta uharibifu kwa jamii, katika kipindi cha Desemba pekee, watu watatu wameuawa na tembo katika maeneo tofauti nchini katika Wilaya za Nzega, Tunduru na Monduli.

Alisema kitendo cha TAWA kumuua simba katika kijiji cha Ngwala wilayani Songwe, ili kunusuru maisha ya watu, kimefanya waonekane kuwa wamekiuka haki za wanyama.

Hata hivyo, alisema jambo hilo limefanywa kwa kuzingatia Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 ambayo haipaswi kubezwa na jamii.

Alisema sheria hiyo inatambua umuhimu wa kulinda maisha ya watu na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu licha ya kwamba mamlaka inatumia mbinu mbalimbali za kudhibiti wanyamapori kuingia kwenye vijiji ikiwamo kuwatishia kwa bunduki.

Munuo alisema mamlaka katika kuimarisha usalama kwa watu na mali zao, ililazimika kuwarudisha wanyamapori hifadhini na katika kipindi cha Januari hadi Desemba, mwaka jana, matukio 993 ya wanyamapori kuvamia maeneo ya wananchi yaliripotiwa katika vituo vya TAWA na simba 36 walirudishwa kwenye hifadhi.

"Kifungu cha 73 cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori kinaruhusu wanyamapori wakali na waharibifu kuuawa ili kulinda maisha ya watu na kifungu hicho hutekelezwa pale tu mbinu zingine zinaposhindikana. Wanyamapori wanauawa endapo mazingira yamelazimika kuokoa maisha ya watu," alisema.

"Tunaomba ieleweke TAWA inafanya kazi kwa kuzingatia sheria, weledi na kujali maisha ya watu na kazi zinazofanywa na TAWA zinafanywa na wataalamu wanaojua majukumu yao kwa mujibu wa sheria," alisema Munuo.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# 2021 uwe wa neema kwenu wasomaji, watangazaji wetu

**HONGERA** kwa mwaka mpya wa 2021 watangazaji na wasomaji wetu wa Nipashe. Tunawapenda na kuwashukuru tunawahakikishia kuwa tutaendelea kuwahudumia na kuwa karibu zaidi nanyi kama Mwanga wa Jamii.

Ni wazi kuwa kila wakati unapoanza mwaka mpya unakuwa ndiyo wakati au fursa ya kutafakari na kuangalia nyuma. Tulipotoka na tunakoelekea 2021.

Sisi pamoja na nyinyi ni muda mwingine wa kuangalia malengo yetu na pia kufurahia mafanikio. Timu yetu ya Nipashe tunafurahi kwa vile tumeendelea kuwa karibu nanyi kwa mwaka mzima, tukiwahabarisha, kuwaburudisha na kuwaelimisha.

Tunawashukuru wasomaji na watangazaji wetu kwa vile mmekuwa sababu ya sisi Mwanga wa Jamii kuendelea kuwapo na tunawaahidi kuwa tutaendelea kuwapa burudani, kuwahabarisha na kuwajuza mambo mengine kemkem na kutimiza kile mnachotaka kutoka kwetu ili kwa pamoja tuendelee kuijenga na kuihudumia jamii yetu.

Kwa sababu yenu, mmekuwa chanzo cha sisi kupata taarifa mbalimbali zilizohusu masuala ya uchumi, siasa, burudani na mengine mengi tuliyoyachapisha na kuyawasilisha kwenu.

Kwa hili tunawashukuru wasomaji wetu na kuwatakia mafanikio kwa mwaka 2021 pamoja na kuzidi kuwakaribisha mwendelee kuwa karibu nasi tukiahidi kuwa tuko pamoja katika gurumu la kuleta maendeleo ya jamii yetu kupitia tasnia ya habari.

Mwaka mpya unatukumbusha kuwa taifa letu na jamii ya Watanzania inatuhitaji kuendelea kusambaza upendo, huku tukijua kuwa tuna mambo mengi ya kufanya pamoja, kuanzia sasa ili kuboresha uchumi, kilimo, afya, utamaduni na teknolojia.

Ni wajibu wetu kushirikiana popote tulipo kufanya Tanzania yetu kuwa mahali bora pa kuishi na kila mmoja wetu anakuwa na nafasi ya kusonga mbele. Ndiyo maana tunaahidi kuendelea kushirikiana katika kufanikisha azma hiyo kupitia jukumu hili la upashanaji habari.

Tunaomba uwe mwaka wa mafanikio kwa familia zetu, shughuli zetu za kiuchumi pamoja na maendeleo makubwa kwa taifa letu ambalo sisi sote tunalipenda na kulitakia mafanikio makubwa.

Ujumbe wetu kwenu ni kuwahimiza kuendelea kujituma, kufanyakazi kwa bidii, kupenda maisha yenu pamoja kuishi bila kukata tamaa hata kama hakuna mafanikio, usiwe tena wakati wa kulalamika na kufikiria mbinu ovu.

Changamoto na wakati mwingine shida zinakuwa nyingi kwa kuwa, kuna kutokuridhika ni lazima kukubaliana na hali hiyo, lakini hakuna kukata tamaa tunafahamu kuwa ni lazima tabu zitaendelea kuambatana nasi na ni jambo lisilokwepeka.

Hata hivyo, tukumbuke kuwa juhudi ndizo zinazoleta mafanikio, tuepuke ushirikina, rushwa, mauaji, wizi na vitendo vya kudhalilisha watoto na binadamu wenzetu wanyonge.

Tukumbuke kushukuru na kuendelea kumtumaini Mungu. Kumshukuru na kuendelea kumsihi kuilinda nchi na kuiepusha na magonjwa hasa corona na maradhi ya virusi milipuko.

Tunawakumbusha wasomaji kuwa maisha yetu yatafanikiwa zaidi iwapo tutatenda kwa haki, kuwa watu wa kiasi pamoja na wenye upendo.

Tunaendelea kuwatakia mwaka mpya mwema wenye mafanikio na baraka tele zinazochochewa na kupenda kusoma na kujiendeleza kifikra.

Yote hayo yanafanyika kupitia mitandao ya habari, magazeti, redio na televisheni ili tuzidi kujenga nchi yenye watu walioelimika na wenye kusaka mabadiliko kupitia usomaji na ufuatiliaji wa habari sahihi na kwa kina.

**HERI YA MWAKA MPYA 2021.**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mwaka huu mpya 2021, uitoe jamii kutoka hadithi ya kuuana

Na Sabato Kasika

**SAFARI** ya miezi 12 inayoanza leo, kwa waliobahatika kuanza huku wakivuta pumzi, kila la heri, tukizidi kuombeana heri ya mwaka mpya.

Kwa wenzetu ambao pumzi zao ziligota mnamo 2020 tuwaombee, maana iko wazi kwamba "kila nafsi lazima ionje mauti."

Wakati mwaka mpya ukiwa unakaribia kuanza, ni vyema kujikumbusha machache yaliyotokea mwaka huu unaomalizika, ambayo ni vyema jamii isiingie nayo katika mwaka mwingine unaoanza hesabu leo.

Hapa nitaeleza machache ambayo yamo katika ripoti ya Jeshi la Polisi yanayohusu mwenendo wa hali ya usalama, pamoja na tathmini ya matukio mbalimbali nchini kwa mwaka huu.

Mkuu wa Operesheni na Mafunzo wa Polisi, Kamishna Liberatus Sabas, katika taarifa yake kwa wanahabari, anasema matukio mbalimbali yanayohatarisha maisha ya watu, yamepungua kwa kiasi kikubwa kuliko mwaka uliotamgulia, 2019.

Akitoa tathmini ya kuanzia Januari hadi mwezi Novemba mwaka jana, anasema vifo vitokanavyo na ajali vimepungua kutoka 1329 mwaka juzi 2019 hadi 1158 mwaka jana, ukiwa ni upungufu wa asilimia 12. 9. Kwa kifupi ni mafanikio ya makubwa ya kupunguza matukio makubwa kwa ubaya.

Anafafanua matukio hayo, ni yaliyokuwa kero kwa wananchi husussani makosa ya kutumia silaha, mauaji, pia ajali za barabarani na kwamba matukio ya kutumia silaha yamepungua kwa kiasi kikubwa wa tofauti na mwaka uliopita.

Mwaka 2019 kulikuwapo matukio 378 ya unyang'anyi wa kutumia silaha, lakini mwaka huu umepungua hadi kufikia matukio 273, huku kukiwapo na hatua mpya kwamba yanayotokea sasa hayahusiani na matumizi ya silaha kama zamani.

Anasema, asilimia kubwa ya matukio ya kutumia silaha yamedhibitiwa kote nchini na sasa yamebaki mauaji yanatokana na hisia kama za ushirikina, wivu wa kimapenzi na watu kujichukulia sheria mkononi.

Niseme, hapo ndipo ninapotaka kujenga hoja yangu kwamba, ingependeza kama hayo yote yangeishia mwaka jana, yakabaki mambo yaliyokwishapitwa na wakati, si ya kuendelea kukumbatiwa, katika dunia ya leo.

Nikianza na hili la kujichukulia sheria mkononi, ni vyema jamii ikatambua kuwa wataalamu wa sheria wanaweka wazi kwamba vitendo hivyo ni kosa la jinai kama yalivyo makosa mengine na ukiukwaji sheria za nchi.

Ujumla ni kwamba, jamii iliyostaarabika daima haiwezi kuendekeza vitendo vya aina hiyo, badala yake inaheshimiana na kama kuna jambo halijakaa sawa, hufuata njia sahihi kulitatua, kuliko mkato wa kukatisha uhai wa wengine.

Wivu wa kimapenzi unaosababisha kuondoa uhai wa mtu mwingine ni miongoni mwa yanayotajwa kama kujichukulia sheria mkononi, hivyo wale wanaoendekeza hayo wayaache yaishie 2020, waanze maisha mapya.

Pia, kuna dai la ushirikina ambalo kimsingi nalo linatutia aibu, kusikia mtu anamuua mwenzake kwa tuhuma kwamba anamloga.

Hapo utasikia dhana inayotawala kwamba kila mwenye macho mekundu ni mchawi, hapaswi kuishi ndani ya jamii. Vitendo vya baadhi ya watu kuua vikongwe wenye macho mekundu kwa madai kuwa ni wachawi vinaonyesha kuwa wanaofanya hivyo bado wanaendekeza mambo yaliyopitwa na wakati.

Nawasifu Polisi kwa kufanikiwa kudhibiti matukio yanayohusiana na matumizi ya silaha kama panga, visu na bunduki kwa asilimia kubwa.

Sasa, yaliyosalia ikiwamo ushirikina, wivu wa kimapenzi na watu kujichukulia sheria mkononi, jamii iyadhibiti.

Wanaokumbutia ushirikiana na mauaji, ni vyema wakabadilika kwa kujiepusha na kuwa na hofu ya Mungu, kwa kuwalinda wazee wenye macho mekundu na kinamama wanaohisiwa wachawi, hali kadhalika wenye ulemavu.

Basi itoshe kwa kumalizia na hoja, 2021 uwe mwaka wa mabadiliko na kuitoa jamii kwenye giza nene linalosababisha imani ya ushirikina na kujichukulia sheria mkononi au watu kuuana kwa wivu wa mapenzi.

# HABARI PICHANI



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mgodi wa Busolwa, Baraka Ezekiel, alipotembelea mgodi huo uliopo Kijiji cha Buhunda, Wilaya ya Misungwi, Mkoa wa Mwanza, juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**



Muuguzi na Mkunga Rukia Balo kutoka Mpendae akiwasilisha mchango wake katika mkutano maalum wa wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii uliofanyika chini ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Hassan Mwinyi (hayupo pichani). **PICHA: MPIGA PICHA WETU**



Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya CRDB nchini, Prosper Nambaya, akimkabidhi Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, kompyuta moja ikiwa ni sehemu ya 100 zilizotolewa na benki hiyo kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Murilo Jumanne, akisalimiana na wavuvi wa mwalo wa Izinga katika Kijiji cha Karumo, wilayani Sengerema, wakati alipofanya doria ya kuimarisha hali ya usalama katika visiwa vyote vilivyomo ndani ya Ziwa Victoria. **PICHA: ROSE JACOB**



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa Kituo cha Malezi kwa Watoto katika Shule ya Msingi Mbagala Kuu, Manispaa ya Temeke chenye lengo la kutoa malezi kwa watoto. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Polisi: Ubakaji bado tatizo Simiyu

**Na Ndalike Sonda,** BARIADI

JESHI la Polisi Mkoa wa Simiyu, limesema vitendo vya ubakaji na mimba kwa wanafunzi bado ni tatizo linalokabili jamii mkoani humo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, Richard Abwao, aliyasema hayo juzi mjini Bariadi alipozungumza na Nipashe kuhusu hali ya vitendo hivyo.

Alibainisha kuwa mwaka 2019, jumla ya makosa 104 yaliripotiwa kwa Jeshi la Polisi huku mwaka 2020 yakiripotiwa matukio 110, sawa na ongezeko la asilimia 5.5.

Alisema uwapo wa vitendo hivyo unachangiwa na jamii kutokuwa na elimu juu ya kukabiliana na suala la mimba shuleni na ugumu wa upatikana kwa ushahidi yanapotokea matukio ya ubakaji.

Kamanda Abwoa alisema jeshi hilo kupitia Dawati la Jinsia na Watoto, wamejipanga kuhakikisha wanapunguza matukio hayo mwaka huu kwa kushirikiana na vyombo vingine, kwa kutoa elimu kwa jamii na kuwajengea uwezo viongozi wa ngazi za vitongoji, vijiji, mitaa na kata ili kila mwananchi awe na uchungu wa kukabiliana na tatizo la ubakaji na mimba kwa wanafunzi.

Alisema jeshi hilo pia limejipanga kukabiliana na matukio ya uhalifu mwaka huu, ili wananchi wakufanye shughuli za maendeleo bila hofu ya wahalifu.

Kamanda Abwao aliwaomba wananchi kusherehekea kwa amani sikukuu ya Mwaka Mpya, akionya kuwa sheria kali zitachukuliwa dhidi ya watakaobainika wanaovunja taratibu.

# Bashungwa atembelea maduka yaliyoungua

**Na Eliud Rwechungura,** KARAGWE

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, amekutana na wafanyabiashara wa mji wa Kayanga na kutoa pole kwa waathirika wa ajali ya moto uliotokea Desemba 26, mwaka jana na kuunguza maduka 10 yenye thamani ya Sh. milioni 190.

Bashungwa jana alikutana na wafanyabiashara hao katika mkutano uliofanyika mji wa Kayanga, Karagwe na baadaye alifuatana na wafanyabiashara hao kutembelea eneo la maduka yaliyoungua.

Waziri huyo alisema mpaka sasa, Wilaya ya Karagwe ina gari la zimamoto mkoani Kagera, lakini amekuwa akipokea taarifa kuwa ni bovu, hivyo kutoa maelekezo kwa mkuu wa wilaya kufanya matengenezo ya gari hilo haraka iwezekanavyo.

"Mimi ndiye niliyepambana kupatikana kwa gari la zimamoto, ukiangalia kwenye Mkoa wa Kagera, wilaya yenye gari la zimamoto ni hapa Karagwe tu.

"Mkuu wa wilaya ninakuamini katika uchapaji kazi, lakini tunapozungumzia kukomesha ajali za moto, tukumbuke na kukomesha ubovu wa gari letu la zimamoto," alisema.

Bashungwa alitumia nafasi hiyo kuwaomba na kuwakumbusha wafanyabiashara wote kukata bima ya moto kwa kuwa hawajui ni wakati upi watakumbwa na matukio ya ajali za moto.

Waziri huyo pia alitoa zawadi ya fedha (Sh. 100,000) kwa askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Koplo Denis Minja, aliyemwokoa mtoto aliyekuwa kwenye shimo la choo siku tatu zilizopita.

Mkuu wa Wilaya ya Karagwe, Godfrey Mheruka, alitoa mapendekezo yatakayosaidia kukokomesha majanga ya moto wilayani Karagwe, akisema:

"Wafanyabiashara waweke walinzi wenye uhakika maana walinzi wengi ni wazee sana na walevi, kila duka liwe na kifaa cha zimamoto ili kusaidia kuzima milipuko kabla haijasambaa zaidi.

"Jeshi la Polisi lisaidiane na walinzi wa kijamii katika ulinzi shirikishi ili kudhibiti uzururaji wa vibaka usiku."



Wananchi wakiangalia gari iliyokuwa ikipita kwenye daraja la miti na kukwama katika eneo la Goba Tegeta A, jijini Dar es Salaam jana. Eneo hilo hakuna daraja la kupita gari. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# DC ashtukia uonevu wa wanafunzi shule binafsi

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Anamringi Macha, amewataka wamiliki wa shule binafsi wilayani humo kutoitumia mitihani ya taifa kama fimbo ya kuwaadhibu wanafunzi wanaoshindwa kulipa ada.

Vilevile, amewataka wamiliki hao kutowasumbua wazazi na wanafunzi mara kwa mara kwa masuala ya ada na michango, akitambua pia mchango wa shule hizo katika kusaidia maendeleo ya elimu wilayani Kahama na Mkoa wa Shinyanga kwa ujumla.

Macha aliyasema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake mjini hapa, akibainisha kuwa mitihani ya taifa ni suala la kiserikali na ni kosa kumzuia mwanafunzi kufanya mitihani hiyo kwa kisingizio cha kutokamilisha malipo ya ada ya shule.

Macha alisema kuna baadhi ya shule zinatumia wakati huo wa mitihani kuwazuia wanafunzi kufanya mitihani kwa vile wengine wanakuwa hawajalipa karo zao za mwaka na kuwarudisha majumbani, jambo ambalo siyo sahihi kisheria.

"Kuna baadhi ya wamiliki wa shule hizo binafsi hutumia muda wa wanafunzi kufanya mitihani ya taifa hasa wale wa kidato cha pili na cha nne, kuwarudisha majumbani kwa vile hawajamaliza kulipa karo zao, jambo hilo halitakiwi kabisa kwani suala la mitihani ya taifa ni la kiserikali," alionya.

Aliwataka wazazi na wamiliki hao wa shule binafsi kushirikiana, akisema kuna baadhi ya shule zingine wamekuwa na tabia ya kuzuia vyeti vya wanafunzi, jambo ambalo pia siyo sahihi.

Macha aliwataka wazazi kuziamini shule zinazomilikiwa na serikali kwa kuwa zinatoa elimu bora na ya kutosheleza kwa wanafunzi ingawa pia kuna shule hizo binafsi ambazo nazo hufanya hivyo hivyo.

Alisema kuwa wazazi wahakikishe wanajipanga na kujipima uwezo wao kama watahimili michango iliyopo katika shule binafsi au la.

Alisema kuwa kama wazazi wanajiweza kifedha, basi wawapeleke watoto wao katika shule binafsi na wakishindwa, waangalie sehemu nyingine ya kuwapeleka ili wanafunzi wapata elimu stahiki.

"Kama kuna mzazi anajiweza kifedha kumpeleka mwanawe katika shule binafsi, basi ampeleke, lakini kama hana uwezo, ahakikishe anampeleka katika shule za serikali kwani nazo zinatoa elimu bora kama ilivyo kwa shule zingine wilayani Kahama," alifafanua.

Kiongozi huyo wa wilaya pia alitoa pongezi kwa shule ambazo zimefanya vizuri katika mitihani ya taifa mwaka jana, zikiwamo zilizotoa wanafunzi wanne bora kitaifa katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi.

HABARI KITAIFA

# Udhibiti uvuvi haramu kuwa endelevu

**Na Happy Severine,**

BUSEGA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema wizara hiyo imejipanga kudhibiti uvuvi haramu na kazi hiyo inakuwa endelevu.

Mashiba aliyasema hayo jana wakati wa ziara yake mkoani Simiyu na kueleza kuwa uvuvi haramu hauna tija na serikali itawakamata wote wanaojihusisha na vitendo hivyo.

Alisema wizara hiyo itahakikisha udhibiti wa uvuvi haramu unakuwa shirikishi wenye kutatoa matokeo chanya na siyo kuishia kukamata vifaa na wavuvi haramu huku akiongeza kuwa lengo kubwa la udhibiti huo ni kumaliza tatizo hilo.

"Zoezi hili litakuwa endelevu badala ya kuwa zimamoto tutashirikiana kuanzia ngazi zote lengo likiwa kuhakikisha tatizo la uvuvi haramu linakwisha ili tupate tija kwenye uvuvi...tutadhibiti kwa kufuata taratibu na sheria za nchi, hatimaye tupate malighafi za kutosha kwenye viwanda tuongeze pato la mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla," alisema Ndaki.

Pia, alisema wizara imejipanga kutoa mchango mkubwa kwenye pato la taifa huku akiongeza kuwa sekta ya mifugo na uvuvi ina rasilimali nyingi ambazo zikisimamiwa vizuri zitachangia pato kwa kiasi kikubwa.

Alisema hakuna sababu ya mfugaji na mvuvi kuwa maskini wakati anazalisha malighafi nyingi zinazohitajika kwenye viwanda hususan vya ndani.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa sekta ya mifugo na uvuvi kwa mkoa wa Simiyu kwa niaba ya Katibu Tawala wa Mkoa huo, Mhandisi Mashaka Luhamba, alisema jumla ya Sh. 282,333,930 zimekusanywa kwenye halmashauri zote sita mkoani hapo ambazo zimetokana na maduhuli ya samaki na mazao yake kwa kutoza leseni, ushuru na faini za makosa mbalimbali kwa mujibu wa sheria na kanuni za uvuvi.

Luhamba alizitaja changamoto hizo kuwa ni pamoja na wavuvi kuvamiwa ziwani na kunyang'anywa mali zao na wakati mwingine kupoteza maisha, ukosefu wa vitendea kazi, uhaba wa watumishi wa sekta ya mifugo na uvuvi na uhaba wa maji na malisho wakati wa kiangazi.

Akijibu changamoto ya wavuvi kuvamiwa na kunyang'anywa mali na wengine kuuawa, Waziri Ndaki alisema serikali haitakubali kuona Mtanzania anapoteza maisha.

"Hatutokubali kuona Mtanzania anapoteza maisha ... mtu yupo ziwani anajitafutia kipato atokee mtu amvamie amuue hii haikubaliki hata kidogo tutahakikisha tunawalinda wavuvi wetu ili waendelee kujitafutia kipato chao cha halali," alisema Ndaki.

Naye Mbunge wa Jimbo la Busega, Simon Songe, alisema kuna matatizo mengi kwenye sekta ya uvuvi huku akiitaja moja wapo kuwa ni tozo nyingi na kuiomba serikali kuzitatua.

Baadhi ya wananchi wameiomba serikali iwasaidie kutatua tatizo la viboko wanaohatarisha maisha yao wakati wa ufanyaji shughuli za uvuvi na watu wanaowavamia na kuwanyang'anya vitendea kazi na wengine kuhatarishiwa maisha yao.



Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Tabia Maulid Mwita, akipokea 'tracksuit' 65 na vifaa vya michezo kutoka kwa Meneja wa NMB anayewakilisha Zanzibar, Abdallah Duchi, kwa ajili ya matembezi yatakayofanyika leo na mashindano ya michuano ya Kombe la Mapinduzi, ikiwa ni shamrashamra za maadhimisho ya kumbukumbu ya Siku ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Kushoto ni Katibu Mkuu, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Omar Hassan King. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kuweka kituo kimoja tozo mifugo, uvuvi

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema ina mpango wa kuwa na kituo kimoja cha kulipia tozo zote za mazao ya mifugo na uvuvi.

Akizungumza na baadhi ya wavuvi katika Kata ya Nyamikoma, iliyopo Wilaya ya Busega, mkoani Simiyu wakati wa ziara yake ya siku moja mkoani humo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema wizara hiyo itaangalia upya tozo hizo, ili kuhakikisha zinazotolewa ni rafiki kwa uwekezaji.

Alisema kupunguza tozo zisizo za lazima itawasaidia pia wafugaji na wavuvi wadogo kunufaika na sekta hiyo.

"Tunaamini kwamba uwapo wa tozo ambazo zitakuwa rafiki katika kukuza sekta za mifugo na uvuvi kutavutia watu wengi kuwekeza katika sekta hizi na kuongeza pato la taifa kwa sababu shughuli za kiuchumi zitaongezeka," alisema Ndaki.

Alisema kwa sasa soko la samaki ni kubwa tofauti na miaka iliyopita na kwamba ni vema wavuvi hao wakaanza kufuga samaki kupitia njia za vizimba na mabwawa ili kujiongezea kipato zaidi. Alisema ni sera ya serikali kuhakikisha katika kipindi cha miaka mitano ajira zaidi zinapatikana kupitia ufugaji wa samaki.

Alimwagiza Katibu anayeshughulikia uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, kuanzisha utaratibu wa kuwapo kwa kizimba cha mafunzo kwa ajili ya kufugia samaki na wataalamu kutoka wizarani wanakwenda vijijini kuwafundisha wananchi namna ya kufuga na kulisha samaki wa kufugwa.

"Sasa hivi soko la samaki limekuwa kubwa sana, kwa sababu hiyo inabidi na sisi wafugaji tubadilike, tusifanye kazi kwa mazoea, tuwekeze kwenye ufugaji wa samaki na serikali iko tayari kuwasaidia hata kwa kuwapatia elimu namna ya kufanikisha hilo na kwa kufanya hivyo mtajiongezea sana kipato," alisema Ndaki.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa wizara hiyo, Pauline Gekul, alisisitiza serikali haita fumbia macho baadhi ya wavuvi wanaoharibu mazao ya uvuvi.

Alisema ni wakati sasa jamii ikashirikiana na serikali kuwabaini watu wanaojihusisha na uvuvi haramu kwa kuwa wanaishi katika maeneo yao na wanayofahamika katika jamii zao ili wachukuliwe hatua kali za kisheria.

## Mongella aridhishwa kasi ujenzi madarasa

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

ILI kuhakikisha wanafunzi wanaotarajia kujiunga na kidato cha kwanza wanapata vyumba vya madarasa, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella na kamati yake ya ulinzi, usalama na wataalamu wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, wamefanya ukaguzi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa na shule mpya.

Akizungumza baada ya ukaguzi wa shule 12 za sekondari zilizopo katika Wilaya ya Nyamagana, alisema kazi iliyofanyika ni kubwa ambayo imemhakikishia wanafunzi wote kuingia kwenye vyumba vya madarasa.

Katibu Tawala Nyamagana, Yonas Alfred na Constantine Sima ambaye ni Meya wa jiji hilo, walisema jitihada zinafanyika ili kuhakikisha wanafunzi wanaingia madarasani.

## Magari Halmashauri ya Tarime kuchunguzwa

**Na Dinna Stephano,** TARIME

KAMATI ya Fedha, Uongozi na Mipango imeanza kuchunguza magari ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ambayo baadhi hayakuorodheshwa kwenye taarifa ya mali za halmashauri.

Kamati hiyo yenye wajumbe 12 akiwamo Mbunge Mwita Waitara, imeanza uchunguzi jana na itakabidhi ripoti Januari 2, mwaka huu, katika kikao cha Baraza la Madiwani kama iliyoagizwa na baraza hilo katika kikao cha Desemba 21, mwaka jana.

Katika kikao hicho kilibaini kutokuwapo kwa baadhi ya mali za halmashauri wakati wa uwasilishwaji wa taarifa ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Apoo Tindwa, ya mali za halmashauri iliyowasilishwa mbele ya baraza hilo.

## Udhibiti njia za panya waongeza mapato

**Na Shaban Njia,** NGARA

UDHIBITI wa njia za panya za utoroshaji wa mazao ya kibiashara na chakula, Halmashauri ya Ngara, mkoani Kagera unasababisha kuongeza mapato ya ndani ya halmashauri kutoka kiasi cha Sh. milioni 760 kwa mwaka hadi kufikia kiasi cha Sh. bilioni 1.5.

Hayo yamebainishwa na mkurugenzi wa halmashauri hiyo, wakati akizungumza na vyombo vya habari ofisini kwake, alisema mwaka 2016, halmashauri hiyo ilikuwa ikikusanya mapato ya ndani kiasi cha Sh. milioni 760 kwa mwaka ni baada ya wananchi kutumia njia za panya kusafarisha mazao ya biashara hasa kahawa kwenda kuuza nchi za Rwanda na Burundi na kusababisha halmashauri kukosa mapato.

# Kalemani akerwa upotevu mamilioni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amesikitishwa na gharama kubwa ya matumizi ya kutoa huduma ya umeme kwa wananchi wa mikoa ya Kigoma na Katavi kutokana na kutumia mafuta mazito kwa ajili ya kuendeshea mitambo ya kufua umeme.

Dk. Kalemani alibainisha hayo mkoani Shinyanga juzi, alipozungumza na watumishi wa Shirika la Umeme (TANESCO) mkoani hapa kwenye kikao kazi alichofuatana na Naibu Waziri wake, Steven Byabato.

Alibainisha kuwa katika Mkoa wa Kigoma, TANESCO imekuwa ikiingia gharama kubwa ya kufua umeme na kuusambaza kwa wananchi kutokana na kutumia mafuta mazito, kwa mwezi wakitumia Sh. bilioni moja, huku wakiingiza Sh. 800,000, hivyo kuambulia hasara.

Waziri huyo alisema kuwa, katika Mkoa wa Katavi, shirika hilo linatumia kufua umeme na kuusambaza kwa wananchi kwa kutumia mafuta hayo mazito kwa Sh. 800,000 kwa mwezi, lakini wanaingiza kiasi cha Sh. 400,000, jambo ambalo alisema ni kulitia umaskini shirika.

"Ninatoa maagizo kuanzia sasa hadi kufika Septemba mwakani, nchi nzima wananchi wote wawe wameunganishwa kutumia umeme wa Gridi ya Taifa na hakuna tena kutumia mafuta mazito, ili kuepuka matumizi makubwa na kuingia hasara.

"Pia, kwa nchi nzima hadi kufikia Juni mwakani, (mwaka huu), wateja wote bila ya kujali wakubwa wala wadogo, wawe wameunganishwa kwenye huduma ya Luku, ili kuepuka upotevu wa mapato sababu ukiwa na Luku tutapata fedha zetu kihalali," alisema.

Naibu Waziri wa Nishati, Byabato, alitoa maagizo kwa mameneja wa TANESCO kuhakikisha kuwa hadi kufikia Januari 31 mwaka huu, wawe wameshawasilisha majina yote ya wateja ambao wanatumia huduma hiyo ya nishati ya umeme kihalali pamoja na kuwafichua wezi wa umeme na kuwachukulia hatua.

Alisema kumekuwapo na idadi kubwa ya watumiaji wa nishati ya umeme kuliko wateja halali, akisisitiza kipindi hiki ni cha kufanya sensa hiyo ili kuwa na idadi kamili ya wateja halali wa shirika hilo na kuwaondoa wanaotumia nishati kwa njia za panya.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Wenye Ulemavu), Ummy Nderiananga (kulia), akimsikiliza Meneja Karakana ya Disabled Aid & General Engineering (DAGE), Henry Chacha (katikati) wakati wa ziara yake ya kutembelea vikundi vya watu wenye ulemavu ambavyo vinajihusisha na shughuli za uzalishaji mali kupitia uwezeshaji wa mikopo inayotolewa na halmashauri. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kijiji chatenga mil. 20/-ujenzi wa madarasa

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

ILI kukabiliana na uhaba wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Msingi Mwanambaya wilayani Mkuranga mkoani Pwani, Kijiji cha Mwanambaya kimetenga Sh. milioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa shuleni huko.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Leila Chaburuma, alibainisha kutengwa kwa fedha hizo jana alipozungumza na Nipashe ofisini kwake.

"Tumetenga Sh. milioni 20 kupitia mapato ya ndani ili kujenga madarasa mawili katika shule hiyo," Chaburuma alisema.

Mwenyekiti huyo aliongeza kuwa, mbali na kujenga vyumba vya madarasa, pia wamejipanga kutatua kero ya uhaba wa madawati katika shule hiyo.

Alisema ofisi yake inampongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Msham Munde, kwa kuwajengea darasa moja katika shule hiyo lililokabidhiwa miezi miwili iliyopita.

Hata hivyo, alimwomba mkurugenzi huyo kuendelea kuiangalia shule hiyo kwa jicho la huruma kwa kuisaidia kutokana na kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi ambao wanatoka katika vijiji mbalimbali.

Alisema kijiji hicho kupitia ofisi yake, pia kimeridhia kujenga jengo la mama na mtoto kwenye zahanati yao Mwanambaya, huku wakijiandaa kujenga wodi ambayo itawawezesha kukabiliana na ongezeko la wagonjwa kutoka katika vijiji vya Mwanadiratu na Mipeku.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Jumanne Bofu, alisema Songas wamefadhili ujenzi wa nyumba ya mganga mfawidhi wa zahanati hiyo, iliyokabidhiwa mwezi uliopita.

# Waziri: Haki itendeke katika ugawaji mirathi

**Na Neema Hussein,** KATAVI

NAIBU Waziri wa Katiba na Sheria, Geofrey Pinda, amewataka watendaji wa wizara yake kutenda haki kwa wananchi hasa katika masuala ya mirathi ambayo yamekuwa na malalamiko mengi.

Alitoa agizo hilo jana alipopokea taarifa fupi kuhusu masuala ya uendeshaji wa kesi na sheria kwa ujumla alipokuwa katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi.

Naibu waziri huyo alisema kumekuwa kukijitokeza matatizo katika mirathi pale mume anapofariki dunia, lakini hali inakuwa tofauti mke anapofariki dunia mke.

Alisema kuna vitu wamekubaliana ikiwamo kurekebisha Sheria ya Mirathi ambayo haijatamka wazi kuwa mrithi wa mali za marehemu ni nani, hivyo imefanya baadhi ya watu kujiingiza ndani ya mali hizo.

Alisema ni muhimu elimu itolewe kwa wasimamizi wa mirathi ili kufahamu cha kufanya juu ya mali hizo.

"Hata sisi tuliopo hapa linatugusa hili, tukifa leo tunaacha migogoro nyuma, ndiyo maana tunahamasisha ninyi ambao angalau kidogo mna elimu na upeo wa kuelewa, muache maandiko ili ukifa ule wosia wako unasomwa pale ili kupunguza hii migogoro," alisema.

Alisema wameshauriana na waziri kwamba, ndani ya miaka yao mitano ya uongozi, wahakikishe hukumu zote zinatolewa kwa lugha ya Kiswahili kutokana na watu wengi kupoteza haki kwa kushindwa kusoma Kiingereza.

"Hatuwezi kuendelea kuhukumu Mtanzania wa Kavuu kwa Kiingereza, ambaye hata Kiswahili tu kinampa shida. Kwa hiyo, hukumu zitatolewa kwa lugha mbili.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, alisema hawaridhishwi na kitengo cha upelelezi, akibainisha kuwa kesi nyingi zikipelekwa mbele, kunaonekana hakuna kosa kwa sababu ya kitengo hicho kutengeneza mazingira ya watuhumiwa kuonekana hawana makosa, hivyo kuachiwa huru.

Alisema kitengo cha upelelezi kisipokuwa vizuri, hakuna haki yoyote itakayotendeka.



Ukurasa 14

MKINDO B

Shule yenye ujasiriamali unaodhibiti mazingira na kulisha wanafunzi wake



Ukurasa 12

NARCO, kampuni kuu ya mifugo yenye mzizi tangu mwaka 1947

BUFE

IJUMAA JANUARI 1, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Hatimaye maisha mapya Waingereza, EU, kila mmoja 'kivyake' kibiashara

**Na Mwandishi Wetu**

MAKUBALIANO ya Uingereza kujitoa katika Umoja wa Ulaya, yalianza kutekelezwa rasmi jana saa tano usiku, baada ya kutiwa saini kuwa sheria.

Wakati mijadala ikitawala, hatua hiyo ya mwisho ambayo imeigharimu Uingereza baadhi ya mawaziri wake wakuu kujiuzulu, msimamo wa dakika za mwisho wa serikali inayoongozwa na Chama cha Conservative ukabaki 'iwe isiwe tunajitoa'.

Bunge la Ulaya hivi karibuni liliunga mkono makubaliano hayo kwa haraka, baada ya pande hizo mbili kufikia maridhiano.


Uingereza inajiondoa katika soko la pamoja la Umoja wa Ulaya na Umoja (EU) wa Forodha, huku mambo yaliyozaa utata katika msuguano huo, ni pamoja na makubaliano ya uvuvi katika ukanda wa bahari ya Uingereza na ushuru wa bidhaa.

Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, amewashukuru wabunge akiwaambia: "Hatima ya nchi hii muhimu sasa ipo mikononi mwetu."

Lakini wapinzani wa hoja hiyo, wanaponda kwamba nchi inaenda kuwa pabaya zaidi kiuchumi, kuliko ilivyokuwa kwenye Umoja wa Ulaya.

Ni makubaliano yaliyofikiwa muda mfupi tu kabla ya siku ya mwisho iliyowekwa (jana) kufanya hivyo, kutoa mwongozo mpya wa kibiashara na uhusiano wa kiusalama baada ya pande hizo mbili kutengana.

Hatua hiyo inatamatisha mvutano wa hoja ndani ya miaka minne na nusu, tangu Uingereza ilipopiga kura ya ndani ya kujiondoa katika Umoja wa Ulaya.



Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, akiwa na Rais wa Umoja wa Ulaya, Ursula von der Leyen. **PICHA: MTANDAO**

**MAMBO YA MSINGI**

Bado kunamaanishwa Uingereza na Umoja wa Ulaya, zinaweza kuendelea kufanya biashara bila ya kuwapo kodi za ziada kuongezwa kwenye bidhaa.

Uingereza ilipiga kura ya kujiondoa kwenye Umoja wa Ulaya, mwaka 2016, lakini ikafanikisha azma ya kutangaza kujiondoa rasmi kwenye Umoja huo Januari 31, mwaka jana.

Hata hivyo, viongozi husika katika makubaliano hayo, walijiwekea hadi mwisho wa mwaka jana, kufikia makubaliano ya kibiashara, yatakayotekelezwa baada ya kujiondoa.

Bado kuna nafasi ya mabadiliko makubwa mbele: Ingawa yaliyofikiwa yanaelezwa makubaliano kuwa mazuri kibiashara, pia kutakuwapo na mabadiliko ya namna watu watakavyosafiri, kuishi na kufanya kazi. kati ya nchi wanachama wa EU na Uingereza.

Hadi sasa, muswada wa siku za usoni wa EU unatarajiwa kuangazia makubaliano ya kibiashara ya Uingereza, na uliungwa mkono katika hatua ya kwanza ndani ya Bunge lake.

Baadaye, Bunge la Seneti la Uingereza lilipitisha muswada huo baada ya kusomwa kwa mara ya tatu na Waziri Mkuu Boris Johnson, anayesema makubaliano hayo yataruhusu Uingereza kufanya mambo kwa namna yao, pia kuwa na biashara huru na EU.

Wabunge wengi wa chama cha pinzani cha Labour, Uingereza walipiga kura kuunga mkono muswada huo, baada ya kiongozi wao, Sir Keir Starmer kutamka: "Makubaliano hata kama ni kidogo, ni bora kuliko kutokuwa na makubaliano kabisa".

Rais wa Tume ya Ulaya, Ursula von der Leyen na Rais wa Baraza la Umoja wa Ulaya, Charles Michel, walitia saini makubaliano husika. ***BBC***

BIASHARA

# NARCO, kampuni kuu ya mifugo yenye mzizi tangu mwaka 1947

## •Yageuka shule kwa wafugaji jirani

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MTU anapoitaja Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), siyo jina geni hata kidogo. Ni kampuni kongwe.

Aidha, mtu huyo anapozungumzia mifugo nchini na hasa ng'ombe, ambao ndio bidhaa kuu wanaopatikana ranchi, hali kadhalika utajiri wa nchi ulikolala, ikishika nafasi ya pili barani Afrika.

Ikirejea historia nchini, ni safari inayoanzia mwaka 1947 ilipoanzishwa kampuni ya kumiliki mashamba ya karanga ya Kongwa, Urambo na Nachingwea, iliyojulikana kwa jina la Overseas Food Corporation (OFC).

Mipawa anasema mwaka 1956, shughuli za OFC zilihamishiwa katika iliyokuwa kampuni ya Tanganyika Agricultural Corporation (TAC) na ufugaji ng'ombe wa nyama ulianzishwa.

Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), Masele Mipawa, alisema NARCO ya leo ilizaliwa katika kilele cha utekelezaji Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Nchi, 1964 hadi 1969; Azimio la Arusha la Mwaka 1967 iliyohimiza miliki ya mali zote nchini kuwa za umma na kuundwa Sheria ya Mashirika ya Umma mwaka 1969.

Kaimu Meneja Mkuu wa NARCO, Masele Mipawa, anasema wakati huo ikijulikana NACO (National Agricultural Company), ilihamishiwa chini ya kampuni tanzu National Agricultural and Food Corporation (NAFCO), kutoka Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC).

Mipawa anasema kabla ya hapo, mwaka 1968 kampuni ilisajiliwa kwa jina la National Agricultural Company, lengo ni kuendeleza na kueneza ufugaji wa mifugo ya nyama, wakati huo ikiwa chini ya NDC.

Anasema, baadaye Oktoba 1974, NACO ilihamishiwa kusimamiwa na kampuni ya LIDA Mamlaka ya Uendeshaji wa Mifugo (LIDA) na mwaka unaofuata ilibadili jina kuwa National Ranching Company Limited (NARCO).

Mipawa anaeleza kuwa, LIDA ilipofungwa na serikali mwaka 1986 na NARCO ilibaki kuwa kampuni inayojitegemea chini ya iliyokuwa Wizara ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo.

### KULIKONI NARCO?

Mipawa anasema, serikali ilianzisha NARCO kwa ajili ya kuendeleza na kueneza ufugaji bora, hususan ng'ombe bora wa nyama kukidhi masoko ya ndani na nje ya nchi kwa kutumia mbinu za ufugaji wa kisasa.



Kaimu Meneja Mkuu wa kampuni ya NARCO, Masele Mipawa (aliyevaa suti nyeusi), alipoongea na wafanyakazi wa ranchi ya West Kilimanjaro.

> **"NARCO, pia imefanikiwa kuzalisha na kuuza kwa wananchi malisho bora na ya uhakika kwa bei nafuu hasa kwa ajili ya wananchi wenye mifugo inayofugwa mijini na wakati wa kiangazi, ambao kunakuwapo uhaba mkubwa wa malisho," anasema Masele.**

Anasema sehemu kubwa ya ng'ombe wanaofugwa ni aina ya Boran, ambao wana umbile kubwa na wana sifa ya kukua haraka, ikilinganishwa na aina ya Zebu, ambao wana tija ndogo katika uzalishaji.

"Pia, NARCO ilianzishwa ili kuwa na chachu ya mabadiliko katika sekta ya mifugo kwa kuwasaidia wafugaji wengi kujifunza kutoka kwenye kampuni na kuiga mbinu mpya za ufugaji wa kisasa na kibiashara," anasema.

Mipawa anasema Tanzania ina jumla ya ranchi 14 zenye ukubwa wa hekta 641,152.51 katika mikoa tisa, akiitaja: Kongwa, Ruvu, Mkata, Dakawa, Kalambo, Kikulula, Misenyi, Kitengule, Uvinza, Usangu, West kilimanjaro, Kagoma, Mabale na Mzeri.

Anasema hadi kufikia Juni mwaka jana, katika jumla ya maeneo hayo yenye uwezo wa kuhifadhi ng'ombe 180,000, kulikuwapo na vitalu vyake vya muda mrefu na mfupi venye ng'ombe 137,801; mbuzi 11,753; kondoo 6,000; nguruwe 144 na farasi 27.

### HATUA YA MAFANIKIO

Mipawa anasema, tangu kuanzishwa NARCO imefanikiwa kusambaza mbegu za mifugo kwa kuwauzia wananchi kwa bei nafuu, ikilinganisha na bei ya sokoni, wafugaji wakinufaika kupata madume na mitamba bora.

Vilevile anasema NARCO imeshatoa mafunzo kwa vitendo kwa vijana 1,000 inayowapokea kila mwaka nchini, kutoka vyuo vya elimu ya juu na kati, mifugo, shule za sekondari na msingi.

Anasema ni mafunzo kwa vitendo na utafiti katika fani mbalimbali za sayansi ya mifugo na kilimo, mazingira, biashara, uwekezaji na ufugaji kisasa na biashara.

Maeneo mengine, anayataja kuhusu utoaji ushauri wa kitaalamu katika kinga na tiba za magonjwa na unenepeshaji mifugo, malisho bora, uzalishaji na uendeshaji shamba la malisho ya mifugo, ranchi ndogo, uhamilishaji, uandaaji na utunzaji nyama bora.

"NARCO, pia imefanikiwa kuzalisha na kuuza kwa wananchi malisho bora na ya uhakika kwa bei nafuu hasa kwa ajili ya wananchi wenye mifugo inayofugwa mijini na wakati wa kiangazi, ambao kunakuwapo uhaba mkubwa wa malisho," anasema Masele.

Anataja mkakati mwingine ni kuimarisha uhusiano mzuri kati yake na wafugaji wanaozunguka ranchi zake, ikiwamo kuwapangisha kwa mikataba mifupi, namna inayowasaidia wafugaji kutohama na mifugo kutafuta malisho na maji.

Hapo anataja takwimu ya kuwapo ng'ombe 31,356, mbuzi 11,733 na kondoo 6,000 kutoka vijiji 30 nchini kote na wameshapata huduma katika ranchi za NARCO, zinazozalisha na kutunza mbegu bora ya ng'ombe, aina ya Boran.

"Serikali imendelea kujivunia zao la Boran na kuhimiza uzalishaji wa madume kwa ajili kuwauzia wafugaji ili waboreshe mifugo yao ya asili tangu kampuni ianze miaka ya 1968 na imekuwa ikizalisha ng'ombe wa nyama aina ya Boran," anafafanua.

Mipawa anasema, wakati wa kiangazi ranchi zake katika mikoa tisa huwanufaisha kwa huduma ya maji zaidi ya wanachi 2,500 na mifugo 30,000 yanayopatikana katika visima na vyanzo vingine bure.

Pia anajigamba, NARCO imefanikiwa kuhifadhi mazingira na malisho ya mifugo, kwani maeneo yote ya ranchi yana malisho ya kutosha wakati wote kutokana na kuzingatia mbinu bora za ufugaji.

Mengine anayataja ni afya bora kwa wananchi, kutokana na bidhaa bora za nyama na maziwa wanayoyatoa kwa soko la wananchi, huku wakati huohuo miradi yake ikifungua fursa kwa umma wa Watanzania.

Anasema, NARCO imeshatoa gawio serikalini na kwa miaka miwili ya kibajeti imeshatoa jumla ya shilingi milioni 400 kwa Mfuko Mkuu wa Serikali.

### MATATIZO MBELE YAKE

Mipawa anasema, shida inayoikabili kampuni ya NARCO, ni uvamizi wa wananchi katika maeneo ya ranchi na kuendesha shughuli zao za kiuchumi, ikiwamo kilimo.

Pia, analalamika kuwapo wananchi wanaovamia maeneo yake wakiendesha mifugo na kufuata maji, hali inayochangia uharibifu wa mazingira, miundombinu kama mabwawa na kuleta magonjwa ya kuambukiza kwa mifugo ndani ya ranchi.

"Katika kuitatua changamoto hii, NARCO ilikuja na utaratibu wa upangishaji vitalu vya muda mfupi, hasa kwa maeneo ya pembezoni mwa ranchi. Kwa kufanya hivyo, imeweza kupunguza uvamizi na kuweka utaratibu mzuri wa ulishaji," anasema.

Anafafanua kwamba, NARCO iliamua kumega baadhi ya maeneo yenye uvamizi mkubwa na kuyagawa kwa wananchi na imeendelea kuweka mipaka na alama za kuonekana katika ranchi zake, ili kuyalinda maeneo yaliyobaki dhidi ya uvamizi.

Pia, anataja ukosefu wa mtaji kwa ajili ya kuendesha shughuli za uendelezaji wa ranchi na ufugaji wa ng'ombe bora na kibiashara, nayo ni tatizo.

Anasema, kampuni imekuwa ikitoa elimu ya kila mara kuhusu umuhimu wa ufugaji bora wa mifugo na faida za kuzingatia uwiano wa maeneo ya malisho na idadi ya mifugo waliopo.

### MPANGO MKAKATI

Pia, NARCO imeendelea kutafuta mitaji na tayari imeshaandaa andiko la mpango wa biashara wa kufufua na kuboresha ranchi nane, kati ya 14 katika awamu ya kwanza na tayari andiko hilo limeshawasilishwa serikalini kupitia Benki ya Kilimo Tanzania (TADB), ili kupata uwzeshaji mkopo wa shilingi bilioni 20.

Anasema, kampuni hiyo ina mikakati wa kuhakikisha inaongeza ukusanyaji mapato kwa kuongeza uzalishaji nyama katika viwanda vinavyotegemea malighafi ya mifugo kama ng'ombe, mbuzi na kondoo.

"Tunatarajia kuingiza mitamba ya kutosha nchini hasa kutoka nchi jirani za Afrika Mashariki, ili wananchi waweze kupata mitamba ambayo imekuwa adimu sana," anabainisha Mipawa.

Wito wake anawataka wafugaji wanaohama, kwamba utaratibu huo umepitwa na wakati na hauna tija katika uzalishaji mifugo kibiashara, wanapaswa kuwa na maeneo ya kuendesha ufugaji na kuyaendeleza, ili kufuga kibiashara.



Sehemu ya ng'ombe wanaofugwa katika moja ya ranchi za NARCO. **PICHA ZOTE: PAUL MABEJA**

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Watanzania tunaweza kuepusha majanga






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

WATANZANIA tunaweza kuwashangaa, kwa jinsi wanavyoendesha maisha yao, hasa linapokuja suala la kutojali wanaishi vipi dhidi ya majanga yanayoweza kuwakuta.

Wao husubiri yawakute kwanza, ndipo huzinduka na kuchukua hatua ya kujikinga au kuzuia. Na hufanya hivi, baada ya kupata hasara ya mali au maisha.

Mara nyingi majanga huwakuta huku wakiwa na uwezo wa kuyaepuka na ndipo wanaowaongoza huja juu na kuwakemea na wakati mwingine hata kuwatukana, kutokana na kilichowakuta.

Yapo majanga ya asili, ambayo si rahisi kuyaepuka na mara nyingine, huwa si rahisi kutabiri kuwa yatatokea. Matukio kama ya matetemeko ya ardhi au volkano, ni ya asili na si rahisi kuotea kuwa yatakuja.

Lakini, angalau mvua hutabirika na kuwezesha hatua za hadhari kuchukuliwa, ili kuepuka majanga. Hata hivyo, yapo ya kujipangia wenyewe binadamu, kwa kutafuta furaha na maslahi na kujikuta yamegeuka kuwa maafa. Siku za karibuni, tumeshuhudia viongozi wakichachamaa kufuatilia vituo vya kulelea watoto wadogo, ambavyo hujulikana kama shule za awali au chekechea, ambako wazazi wengi hususan wa mijini kufanya watoto wao kuwaandaa kabla ya kuanza shule za msingi.

Hatua hiyo imekuja bada ya shule moja kuangukiwa na ukuta wa uzio, ambao ulikuwa ukijengwa jirani nayo na kusababisha baadhi ya watoto wa kituo hicho kupoteza maisha na mmiliki wake kutiwa msukosuko.

Hiyo ilitokana bila shaka na mazingira ya kilipo kituo hicho, ambacho kwa vyovyote vile, ni nyumbani ambako mmiliki huyo katika kutafuta ujasiriamali, akaamua kujenga banda na kukifanya kituo cha kufundishia watoto hao.

Ujasiriamali ndiyo hasa dhana ambayo imekuwa ikisumbua Watanzania wengi, hata kujikuta wakianzisha miradi kama hiyo, si kwa ajili ya kufundisha bali kujipatia kipato.

Mathalan hutokea, kwamba fulani alikuwa mwalimu, baada ya kustaafu akaona ni bora aanzishe kituo cha kulelea watoto na kutafuta mwalimu wa kuwafundisha na kuwapa uji na ikiwezekana maziwa, ili wakue wakisubiri kuanza darasa la kwanza.

Watoto wanakuwa hapo kwa mwaka au miwili, zaidi wakijifunza kuongea Kiingereza, kwa kuwa Kiswahili ni lugha ya nyumbani na mtoto ajuapo 'Good Morning Maza, Faza na Ticha', basi tayari ameiva kuanza shule ya msingi.

Vituo hivyo vimechipuka karibu katika kila mji nchini na sasa umekuwa mtindo na hata kufikia kuamuliwa kuwa mwanafuzni asianze darasa la kwanza bila ya kupitia chekechea, inafanyika na haikwepeki.

Katika wimbi hilo, hapana uhakika kama hata vituo hivyo vimekuwa vikikaguliwa mara kwa mara, ili kuthibitisha ubora wake na kujiridhisha kama kweli wanaofundisha ndio hao na kinachofundishwa ndicho hasa kitakiwacho.

Imekuwa kama ada, kwamba ukaguzi hufanyika pale tu linapotokea la kutokea, ndipo utasikia wamekwenda polisi, zimamoto na wakaguzi wa ustawi wa jamii kama si wa elimu, kwanza kujionea kilichotokea na pili kuhakikisha kama kituo kilistahili kuwapo.

Ndio ugonjwa tulio nao Watanzania, litokee kwanza ndipo tufumbue macho, tuchukue hatua, tutoe matamko na kutunga sheria ndogo, ambazo pia huwa na nguvu za soda na hatimaye hupotea na maisha kuendelea.

Mifano ipo mingi ya kuacha kwanza ajali itokee ndipo hatua zichukuliwe. Tunafanya kazi kwa mazoea tu. Nani anakagua shule kama ilivyokuwa zamani?

Nani anajua nchi ina vituo vingapi vya kulelea watoto wetu, na viko wapi na nani anaviendesha? Kimoja kimeangukiwa na ukuta na kuua, ndipo tunafunua macho na kuacha viti ofisini, kukimbilia eneo la tukio na kutoa matamko!

Je, nani anajua kuwa siku hizi mijini vibandaumiza vya kuangalia ligi za soka za Ulaya na kwingineko vimejiotea kama uyoga? Nani anajua mazingira ya vibanda hivyo, usalama na hatari zao nani anajua?

Bila shaka tutasubiri siku ya siku, moja ya vibanda kiporomoke au kiwake moto, ndipo tutainuka huko ofisini na kukimbilia eneo la tukio kusikitika, na kuandaa matamko ya ukaguzi wa vibandaumiza. Mpo? Alamsiki!

BIASHARA

MKINDO B

# Shule yenye ujasiriamali unaodhibiti mazingira na kulisha wanafunzi wake

**Na Beatrice Philemon**

SHULE ya Msingi Mkindo B iliyopo katika Kijiji cha Bungoma, umbali wa kilomita 35 kutoka Wilaya ya Mvomero, baada ya kugundua umaskini kuwa mwiba kwake katika mlo na mazingira, imeamua kuchukua hatua.

Hatua hiyo ni kubuni mradi wa ufugaji samaki aina ya sato, perege, ikienda sambamba na kilimo cha mihogo na migomba na upandaji miti ya matunda na kupatia kipato cha kusaidia wanafunzi kupata chakula shule na kuboresha taaluuma.

Uanzishaji miradi kama sehemu ya jamii kujifunza, ili kujipatia kipato kuboresha mazingira ya shule kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Pia, watoto kuhamasisha wazazi kujikita katika upandaji miti ya matunda na mbao, katika maeneo wanayoishi ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Fedha zinazopatikana kutokana na uuzaji samaki, mihogo, ndizi, matunda na mbao zinatumika kutekeleza miradi ya maendeleo shuleni na kutatua changamoto inazowakabili katika eneo la shule hiyo iliyoanzishwa mwaka 2005, ikiwa na wanafunzi 1147, kati yao 561 wavulana na wasichana 586.

Mwalimu Mkuu Yusufu Mdetere, anasema mradi huo unaoitwa 'Eco School Programme' umeleta mabadiliko shuleni kutoka kwa wanafunzi wanashiriki kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mradi huo ulianza rasmi shuleni Mkindo B mwaka 2016 kwa ufadhili wa serikali ya Denmark, kupitia shirika lake la Danish Outdoor Council (DOC).

Mpaka sasa mradi unatekelezwa na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), kwa kushirikiana na kamati ya 'Eco-School' inayojumuisha wanafunzi, wazazi na mkuu wa shule.

**MRADI ULIOKO SHULENI**

Mwalimu Mkuu Mdetere, anazungumzia mradi wa ufugaji samaki, kwamba: "Mpaka sasa shule imechimba bwawa la ufugaji samaki katika eneo la shule na tunafunga samaki aina ya sato na perege kwa wananchi wanaopenda kununua samaki kutoka shuleni kwetu."

Anasema Januari mwaka jana, shule ilinunua vifaranga vya samaki kutoka Shule ya Msingi Digalama na kuanza kufuga na hadi Septemba mwaka jana, walifanikiwa kuvuna samaki 100 waliouzwa na kupata Sh. 57,000.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mkindo B, iliyoko Mvomero, Yusuph Mdetere, akielezea jinsi mradi wa ufugaji samaki na upandaji miti, unavyowasaidia kukabili mabadiliko ya tabianchi na kuongeza kipato shuleni. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

Mwalimu Mdetere anasema, fedha zilitumika kununua vifaranga 127 vya sato, kuupanua mradi kwa ajili ya kuongezea shule kipato na wakati huo huo, kusaidia wanafunzi kula samaki. Mapato yalitumika kutekeleza miradi ya shule.

"Tunaishukuru TFCG na serikali ya Denmark kwa kutuletea mradi huu katika shule yetu kwa sababu, tumepata mafanikio makubwa hasa katika eneo la taaluma. Ufaulu umepanda sana tofauti na miaka ya nyuma, utoro pia umepungua kwa sababu chakula kinapatikana shuleni," anasema.

Mwalimu Mkuu anasema, awali watoto wengi walitoroka shule kwa sababu ya njaa, lakini sasa wameacha na mwamko wa wazazi unaongezeka kila kukicha, kwa sababu wanakijiji wa Bungoma hufika shuleni kujifunza na wengine wanachukua miti na migomba kwenda kupanda mashambani mwao.

Kupitia mradi huo, watoto wanaelezwa kujifunza mengi katika eneo la uhifadhi wa mazingira, ufugaji samaki na upandaji miti ya matunda, kivuli na mbao.

Pia, kuna matunda chanya idadi ya wanaofaulu kwenda kujiunga na shule za sekondari imeongezeka na mazingira ya shule yameboreka.

Mwalimu wa Mazingira shuleni Mkindo B, Geofrey Mnari. Anafafanua: "Kama shule tumepanda miti na miti iliyopo ni miti ya mbao, vivuli na matunda na tunaendelea kupanda."

Hadi sasa kuna jumla ya miti ya vivuli 248 kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, pia miti ya mbao 355, matunda 235 zote zinasaidia kuzuia upepo mkali na kuongezea kipato, badala ya kutegemea ukataji misitu.

Mbali na hilo, anasema kuna miche ya migomba 526 imeishapandwa katika ekari moja ya shamba kuwasaidia wanafunzi kupata chakula shuleni, pia kipato.

"Tumepanda miti hii na mazao mengine kama sehemu ya jamii kujifunza na watoto wenyewe wanahamasisha wazazi kupata miti na wazazi wengi wamepanda miti ya matunda," anasema.

Anaongeza: "Wanasema miti ya matunda itawasaidia kula matunda, ila kama shule tunawahamasisha pia kupanda miti ya mbao."

**WANAFUNZI WAWAJIBIKA**

Utaratibu uliopo shuleni, kila mwanafunzi ana utaratibu kila mtoto ana mti wake shuleni, ukiwa katika mfumo umeandikwa jina lake, isipokuwa kwa wanafunzi wa madarasa ya kwanza na chekechea.

"Tumeamua kuanzisha mradi wa mabadiliko ya tabianchi kwa sababu wananchi wengi katika kijiji cha Bungoma wanategemea sana misitu kwa ajili ya uchomaji mkaa na upasuaji mbao, ili kujiongezea kipato," anasema Mwalomu Mnari.

Anasema ukataji misitu katika Hifadhi ya Mkingu, umechangia kwa kiasi kikubwa mabadiliko ya tabianchi katika kijiji cha Bungoma na hivi sasa kuna joto kali sana, vyanzo vya maji vipo hatarini kukauka na miundombinu ya shule, mabati yaliezuliwa.

"Mto Mkindo ambao unatiririsha maji Mto Wami yamepungua sana na upo katika hatari ya kukauka... wananchi wengi wa Wilaya ya Mvomero wanategemea mto huo kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na shughuli za uvuvi," anasema.

**WITO KWA UMMA**

Anatoa rai mradi wa Eco-school, uwageukie wananchi waangalie njia nyingine za kujiongezea kipato, badala ya kutegemea msitu.

Wahusika wanashauri kutumia mkaa mbadala, badala ya kutegemea kukata miti, hali inayohatarisha kuelekea jangwa miaka ijayo.

Mbali na hilo walimu na wazazi waone umuhimu wa mradi huu kwa sababu imepunguza utoro, akifafanua: "Zamani mahudhurio yalikuwa asilimia 70 hadi 77 sasa hivi utoro umepungua kutoka asilimia 60 hadi 95."

Mwalimu huyo ana ufafanuzi, kwamba awali kuna watoto ambao hawakuweza kufika shule hata wastani wa mwezi mzima, sasa hivi mahudhurio yako juu kati ya asilimia 92 na 95 ya wanafunzi wote.

**MJUMBE WA MIRADI**

Mjumbe wa Kamati ya Mradi wa Eco-school, Zuberi John, anasema baada ya kupata ujuzi shuleni, hivi sasa amepanda miche ya michungwa 10, miembe mitatu na huwa anafika shuleni kuwasaidia watoto kuchimba mashimo ya kupanda migomba.

Pia, hivi sasa kunaelewa kuwapo wanakijiji wameanza kufuga samaki na kilimo cha migomba katika mradi huo wa wanawake wanaopewa kipaumbele.

Mjumbe kutoka Kamati ya 'Eco-school', Christopher Ngaleni, anaeleza hatua iliyopigwa: "Tumefanikiwa kuwa na mazingira mazuri, tofauti na zamani. Mwanzoni shuleni hapakuwapo na miti ya vivuli, matunda na mbao,hivi sasa mazingira ya shule yanavutia."

Anaeleza ushindi unakuwapo kwa mzazi kujifunza kutoka shule na kwenda kupanda migomba, michungwa na , kokomanga majumbani kwa ajili ya biashara na matumizi ya nyumbani.

Mwenyekiti wa Kamati ya Eco-School, Bertha Kalyelye, anasema mradi umeisaidia jamii, pia kujenga uhusiano mzuri na shule, umesaidia kuboresha mazingira katika eneo la shule kwa kuwa na miradi midogo na kuboresha taaluma.

Huku anasema kupitia mradi, shule imefanikiwa kuanzisha shamba la migomba na mihogo na wanafunzi wanakula kwa awamu na kufanya kuhudhuria masomo vizuri, tatizio lililopo sasa ni eneo dogo la shule.

Anaendelea: "Watu wanakuja kuiba samaki na mazao mengine ila kuanzia Januari wazazi wataanza kuchanga ili miradi isiishie njiani na watoto wanufaike na mradi."





# Polisi yawahakikishia wananchi Mwaka Mpya wa amani, utulivu

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, amesema wamejipanga kuhakikisha mwaka mpya unasherehekewa kwa utulivu, huku akipiga marufuku disco toto.

Pia amewaonya madereva watakaoendesha magari wakiwa wamelewa watauanza mwaka vibaya.

Muroto, aliyasema hayo jana jijini hapa wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu sherehe za mwisho wa mwaka.

Alisema kuna askari 494 wamepangwa kwa ajili ya doria kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo makanisani, nyumba za starehe, doria za magari na pikipiki na kwenye vizuizi vya kutoka na kuingia Dodoma kwa lengo la kuhakikisha mji unakuwa salama na hakuna matukio ya kihalifu.

"Kuna askari wa kutosha kwenye barabara, madereva wanatakiwa kuhakikisha wanatii sheria bila shuruti, kama unakwenda kwenye ulevi acha gari nyumbani, ukiendesha gari ukiwa umelewa utauanza mwaka vibaya," alisema.

Aliwataka madereva wa matrekta katika mji mdogo wa Kibaigwa Wilaya ya Kongwa kuacha kuingiza barabarani matrekta ambayo hayana taa ili kuepuka ajali.

"Disco toto na habari za mikusanyiko ni marufuku kwa sababu za kiusalama, sehemu zote za starehe zinatakiwa kuwa na wasimamizi kwa ajili ya watoto wakati wakiogelea kwa usalama wao," alisema.

Kadhalika, alisema ni marufuku kuchoma matairi barabarani na atakayefanya hivyo atachukuliwa hatua za kisheria.

"Wanaopiga fataki kuna waliopata vibali na wengine wamenyimwa kama hujapata kibali achana na kupiga fataki," alisema.

Alisema watafanya mkutano na wenye maeneo ya starehe ikiwamo hoteli kwa lengo la kuimarisha usalama kipindi cha sikukuu ya Mwaka Mpya.

"Kila kanisa litakuwa na askari wa kutosha kwa ajili ya kulinda usalama," alisema Muroto.




Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufani Mkoa wa Dodoma, Dk. Ernest Ibenzi (kushoto), na Mjumbe wa Bodi ya hospitali hiyo, John Mchenya (kulia), wakipita eneo la mapokezi la hospitali hiyo, walipokuwa kwenye ukaguzi wa maeneo na utoaji huduma, jana jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Hospitali yaongeza utoaji huduma za maabara

**Na Ibrahim Joseph,**

DODOMA

HOSPITALI ya Rufani Mkoa wa Dodoma imeongeza maeneo ya utoaji huduma za maabara na jengo la upasuaji ili kuendana na ongezeko la wagonjwa wanaofika kupata huduma.

Katika mwaka 2020, hospitali hiyo imefanikiwa kutoa huduma za matibabu ya kibingwa ya upasuaji mifupa, ya mama na mtoto, uzazi na magonjwa ya ndani.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Ernesti Ibenzi, alibainisha hayo jana wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini hapa kuhusu uboreshaji wa huduma katika mwaka 2020.

Alisema, hospitali hiyo imeboresha na kupanua huduma za maabara pamoja na jengo la upasuaji kutokana na ongezeko la wagonjwa wanaofika kupata huduma.

Alisema, hatua hiyo imetokana na maabara kuu ya hospitali hiyo kuzidiwa na sampuli nyingi za wagonjwa zinazochuliwa kwa wagonjwa pamoja na kupunguza mzunguko kwa maeneo ya utoaji huduma ndani ya hospitali.

Aliyataja maeneo ambayo upanuzi huo wa maabara ndogo, ulifanyika kuwa ni eneo la jengo la bima, magonjwa ya dharura, jengo la mama na mtoto pamoja na maabara kuu itaendelea kutoa huduma hizo.

Alisema, kutokana na upanuzi huo kwa sasa hospitali hiyo itakuwa na uwezo wa kuwafanya upasuaji zaidi ya 15, kwa siku moja na kitengo cha mifupa kinauwezo wa kufanya operesheni zaidi ya 150, kwa wiki.

Kadhalika, alisema hospitali hiyo imepanua jengo la kutoa huduma za upasuaji kutoka vyumba vitano vya awali hadi tisa na ukarabati huo umegharimu Sh. milioni 60, ambazo zimetolewa na serikali.

Pia alisema wameboresha huduma za mashine za mionzi (X-ray), ambayo inauwezo wa kutoa majibu ya picha ya mgonjwa kuanzia dakika tatu hadi tano tofauti na ya awali ilikuwa ikitumia dakika 15 na zaidi.

Alisema, hospitali hiyo kwa sasa inahudumia wagonjwa 900, hadi 1,200, hapo nyuma walikuwa wakipokea wagonjwa 300 hadi 400.

# BAKWATA yaomba wazazi kusaidia walimu madrasa

**Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Baraza Kuu la Waislamau Tanzania (BAKWATA), Wilaya ya Dodoma, Bashiru Husseni, amewataka wazazi na walezi wa dini ya Kiislamu kuwasaidia walimu wanaofundisha elimu ya dini hiyo katika madrasa ili wajikwamue kiuchumi.

Alitoa ushauri huo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma baada ya kubaini miongoni mwa walimu wa vituo vya madrasa, hali zao kiuchumi ni ngumu na wanatakiwa kusaidiwa kifedha na mali.

Mwenyekiti huyo alisema miongoni mwa walimu hao hali zao siyo nzuri kiuchumi na kwamba wazazi na walezi wa dini ya kiislamu wanatakiwa kuwajibika kuhakikisha wanasaidia kwa kuwapatia michango mbalimbali.

Hata hivyo, aliwashauri pia masheikh na maimamu wa misikiti kuwahamasisha waumini wao kuwa na moyo wa kupenda kujitolewa kutoa misaada mbalimbali, ili iwasaidie walimu hao ambao wamekuwa na mzigo mkubwa wa kuelimisha watoto katika maadili ya Kimungu.

"Mimi kama Mwenyekiti wa Halmashauri ya BAKWATA Wilaya ya Dodoma, ninawaomba ndugu zangu wa dini ya kiislamu na hata wale ambao siyo Waislamu, toeni misaada yenu mbalimbali ili iwasaidie hao walimu wetu wa vituo vya madrasa," alisema.

Aliwataka masheikh ndani ya misikiti kutumia nafasi zao kuwahamasisha wazazi na walezi wenye watoto wanaosoma na wale waliofaulu kwa mwaka huu kila mmoja kusiwapo na sababu ya kukaa nyumbani.

"Kila mzazi na mlezi hakikishe mtoto wake anampeleka shule kupata haki yake ya kimsingi, ukizingatia kuwa serikali yetu tukufu imetupunguzia mzigo wa kusomesha, hivyo tutumie fursa hiyo ya kusaidiwa na serikali watoto wetu waende shuleni," alisema.

Aliwataka masheikh pamoja na viongozi wa dini wahakikishe wanatumia majukwaa ya nyumba za ibada kusisitiza wazazi na walezi wanawajibika kwa kiasi kikubwa kuisaidia serikali kuhakikisha hakuna mtoto aliyefaulu elimu ya msingi anabaki nyumbani.





## Mwananchi aipa mabati serikali ujenzi madarasa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UONGOZI wa Mkoa wa Mbeya, umepokea msaada wa mabati 120 kutoka kwa mdau wa maendeleo, Ndele Mwaselela, kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari unaoendelea, ili wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza, waanze mapema.

Akipokea mabati hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema mabati hayo yatagawanywa kwenye halmashauri mbili ambazo ni Jiji la Mbeya na Wilaya ya Mbeya.

Alisema lengo la mkoa huo ni kuhakikisha vyumba vya madarasa vinavyohitajika, vinakamilika kabla ya Januari 10, mwaka huu, ili kuwahi muda ambao wamepewa na Waziri Mkuu kukamilisha vyumba hivyo.

Chalamila alisema mkoa huo unahitaji vyumba vya madarasa 100 kwa ajili ya wanafunzi zaidi ya 5,000 na kwamba ujenzi unaendelea kwa kasi katika maeneo yote yenye shule zenye uhaba.

"Ninakushukuru sana Mwaselela kwa mchango wako maana tunataka tuende na mwendo mkubwa, ili tumalize kazi hii mapema zaidi. Sasa, mimi ninapokea kwa mikono miwili na ninamkabidhi Mkuu wa Wilaya ili akawagawie wakurugenzi wake," alisema Chalamila.

Alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, kugawa mabati hayo katika halmashauri zote mbili kulingana na mahitaji, huku akitaka mabati hayo yakatumike ipasavyo.

Aliwaomba wadau wengine kujitokeza kutoa michango yao, ili kuisaidia serikali kukamilisha ujenzi wa vyumba hivyo vinavyohitajika pamoja na miundombinu mingine ya shule.

Akizungumza wakati wa kukabidhi mabati hayo, Mwaselela alisema yeye ni miongoni mwa waumini wa mazingira bora ya elimu nchini kwa ajili ya kuwavutia wanafunzi kujisomea kwa bidii kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Mwaselela ambaye ni mmiliki wa Shule za Patrick Mission ya jijini Dar es Salaam na Paradise Mission ya mkoani Mbeya, alisema yeye ni mzaliwa wa Mbeya na ni miongoni mwa watu waliosoma kwa shida, hivyo hataki wengine wasome kwenye mazingira magumu.

Alisema kuwa mbali na kutoa mchango huo, pia amekuwa akiwasaidia watoto wanaotoka kwenye mazingira magumu kusoma kwa kuwalipia ada, sasa anasaidia watoto 60 wa mkoa huo.

"Tukitoka hapa tunaenda kwenye harambee ya kuchangia ujenzi wa vyumba vya madarasa. Kwa hiyo, hatutaishia hapa, bali tutaendelea kushirikiana kwenye shughuli zingine za maendeleo," alisema Mwaselela.

Aliiomba serikali kuwashirikisha wadau kwenye miradi mbalimbali ili itekelezwe kwa kasi zaidi kuliko inavyofanyika kwa sasa na kwamba kuna watu wana fedha nyingi lakini hawashirikishwi kwenye shughuli hizo.

Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Amede Ng'wanidako, alisema atahakikisha anasimamia vizuri ujenzi wa vyumba vinavyohitajika ili wanafunzi waanze



Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, akipandisha mlima baada ya kukagua mradi wa maji wa Lupata wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya, juzi, mradi huo ulimkera kutokana na kutelekezwa zaidi ya miaka mitano, huku zaidi ya Sh. milioni 30 zikiwa zimeshatumika kuujenga. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Vigogo wa mamlaka za maji watangaziwa kiama

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

NAIBU Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, amesema wizara hiyo itaanzisha operesheni maalum ya 'kuwatumbua' mameneja wote wazembe wa Mamlaka ya Usambazaji Maji Vijijini (RUWASA) wa Wilaya na kuajiri wapya wenye uwezo wa kusimamia sekta ya maji.

Aliyasema hayo juzi wilayani Rungwe mkoani Mbeya, alipokuwa kwenye ziara ya kukagua miradi ya maji, akibainisha kuwa kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuhusu huduma ya maji, huku mameneja hao wakitoa taarifa za uongo kuhusu miradi.

Mahundi alisema asilimia kubwa ya mameneja hao ni wale waliokuwa wakuu wa idara za maji kwenye halmashauri kabla ya kuanzishwa RUWASA na hivyo wanafanya kazi kwa mazoea, jambo ambalo alisema hawezi kulivumilia.

Alisema serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya miradi ya maji, lakini viongozi hao wanashindwa kuisimamia kwa ufasaha na hivyo kutoleta matokeo chanya kwa wananchi ambao huwa wanaitupia lawama serikali.

"Kama umetoka huko na umekuja huku, badilika uendane na mdundo wa huku. Wizara hii haiko tayari kumvumilia mzembe yeyote na tuko tayari kuanza na ma-DM (mameneja wa wilaya) wapya na wenye uwezo wa kufanya kazi vizuri na sitawavumilia," alionya.

Mahundi alisema wapo baadhi ya vijana ambao wako chini ya hao mameneja na wana uwezo mkubwa, hivyo wizara hiyo inaweza ikawapandisha vyeo na kuwapeleka mameneja hao kwenda kuwa mafundi wa kawaida. Akiwa wilayani Rungwe, Mahu

ndi alitembelea miradi mitatu ya Masoko Group unaotarajiwa kuhudumia vijiji 13, mradi wa maji wa Kijiji cha Lukata katika Halmashauri ya Wilaya Rungwe na mradi wa Kandete uliopo katika Halmashauri ya Busokelo.

Katika miradi hiyo aliridhishwa na mradi mmoja pekee wa Masoko Group na katika miradi mingine alibaini upungufu unaotia kichefuchefu, hali iliyomtia hasira na akatishia kumtimua kazi Meneja wa RUWASA wa wilaya hiyo.

Baadhi ya viongozi wa Wilaya ya Rungwe, waliwaomba viongozi wa kitaifa kutoziamini taarifa wanazosomewa na wataalamu wa maji kwa maelezo kuwa nyingi huwa ni za uongo na hivyo wanatakiwa kwenda kwenye miradi moja kwa moja ili kujiridhisha.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Busokelo, Anyosisye Njobelo, alisema wataalamu hao huwa hawasikilizi kero za wananchi na badala yake huwa wanakaa ofsini na kula mishahara ambayo hawaitolei jasho.

Alisema katika Halmashauri ya Busokelo, kuna miradi ambayo wataalamu huwa wanaeleza kwenye karatasi kuwa imekamilika, lakini ni uongo na wananchi hawanufaiki nayo licha ya kutafuna fedha nyingi.

"Kuna mradi kule Busokelo wananchi waliwashauri wataalamu eneo ambalo linafaa kuweka chanzo, lakini hawa wataalamu kwa kukosa busara, walijenga chanzo sehemu nyingine na maji hayatoki, sasa hivi wanataka fedha zingine ili wahamishe," alisema Njobelo.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, alisema Wilaya ya Rungwe ni miongoni mwa wilaya zenye vyanzo vingi vya maji, lakini wananchi wanapata shida kutokana na uzembe wa wataalamu.

Alisema kuna baadhi ya miradi ilianza siku nyingi na hata yeye aliikuta wakati anaanza kazi wilayani humo, lakini mpaka sasa, haina faida kwa wananchi kwa sababu ina matatizo mengi ikiwamo kukosewa tangu mwanzo.

# Vijana mbaroni tuhuma kunaswa na mali za wizi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linawashikilia vijana wawili wakazi wa Mtakuja, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya kwa tuhuma za kukutwa na mali za wizi.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, katika mkutano wake na waandishi wa habari jijini hapa juzi, aliwataja vijana hao kuwa ni Vesto Timoth (18) na Michael Mwile (18).

Alidai vijana hao walikamatwa na kiambaza (screen) moja ya wizi ambayo hakueleza mahali wanakodaiwa kuiiba, lakini akasisitiza upelelezi unaendelea kabla ya kuwafikisha mahakamani. "Tunaendelea na operesheni mbalimbali za kuwasaka wahalifu wote ndani ya mkoa wetu, kwa yeyote mwenye nia ya kufanya jambo lolote la uhalifu ndani ya mkoa wetu, aache mchezo huo maana tutamshughulikia ipasavyo," alionya. Kamanda Matei alisema kuwa, kuelekea sikukuu ya Mwaka Mpya, wananchi hawaruhusiwi kusherehekea sikukuu hiyo kwa kufanya matukio ya uvunjifu wa amani ikiwamo kuchoma magurudumu barabarani.

Alisema mtu yeyote atakayekamatwa kwa kushiriki vitendo hivyo, atachukuliwa hatua za kisheria kama wahalifu wengine huku akiwataka madereva wa vyombo vya moto kuzingatia sheria za usalama barabarani.

Alisema jeshi hilo litaimarisha ulinzi kwenye maeneo mbalimbali ndani ya mkoa huo, ili kuhakikisha wananchi wanasherehekea kwa amani na utulivu. Aliwataka wananchi wanapoondoka majumbani mwao kwenda kusherehekea, kuhakikisha angalau mmoja anabaki kwa ajili ya ulinzi kwa maelezo kuwa wezi wanaweza wakautumia mwanya huo kufanya uhalifu.



# Hemed awataka wabadhirifu kujitathmini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema lazima fedha za serikali ziheshimiwe na mtendaji wa umma analazimika kujitathmini katika kudhibiti mapato ya serikali.

Alisema jicho lake linaangaza katika Bandari Kuu ya Malindi, ili kuhakikisha mapato yanayokusanywa katika eneo hilo muhimu ambalo ni lango kuu la uchumi yanakuwa salama.

Alisema hayo baada ya kusikiliza kero na changamoto zinazowakabili wafanyakazi wa Shirika la Bandari Zanzibar, waliomwomba wakutane naye alipofanya ziara ya ghafla juzi na kuahidi kutekeleza ombi lao. Hemed alisema wakati bandari inalazimika ifanye vyema katika kuiongezea mapato serikali, uongozi wa Shirika la Bandari una wajibu wa kuhakikisha haki za watendaji wake zikiwamo posho za muda wa ziara zinatolewa na kulipwa kwa wakati.

Makamu wa Pili huyo alisema katika kuona ufanisi wa kazi za bandari unaongezeka, uongozi wa shirika hilo utalazimika kutoa ripoti ya changamoto zilizopatiwa ufumbuzi ndani ya mwezi mmoja ifikapo Januari 30.

Hemed alisema kinachohitajika kwa viongozi na watendaji wa shirika hilo ni kuendelea kushirikiana ipasavyo na kuepuka ubinafsi unaojenga kiburi.

Pia alimtaka Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari kulifanyia kazi agizo la Rais Dk. Hussein Mwinyi kwa kupita katika vitengo mbalimbali vya shirika hilo ili kuelewa changamoto zinazowakabili.

Alisema pale atakapobaini yuko mtendaji anashindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa kanuni, taratibu na sheria za utumishi wa umma, ana haki na wajibu wa kumchukulia hatua, vinginevyo wimbi hilo litamwelekea yeye.

Wakitoa malalamiko yao, wafanyakazi wa Shirika la Bandari walisema ucheleweshaji wa malimbikizo yao ya posho umekuwa ukipunguza ari ya uwajibikaji.

Wafanyakazi hao waliomba pia kupatiwa mafunzo kwa lengo la kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi sambamba na upatikanaji wa bima ya afya kwa wakati.

Naye Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Rahma Kassim Ali, aliahidi kwamba muundo wa shirika la bandari ambao umetengenezwa kwa kushirikisha wawakilishi wa vitengo vyote ambao umesharidhiwa na serikali ataufuatilia kwa ajili ya kuanza kufanya kazi.

## SMZ yateketeza tani 52 mchele mbovu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TANI 52 za mchele ambao haufai kwa matumizi ya binadamu, zimeteketezwa katika dampo la Kibele Wilaya ya Kati Unguja.

Mchele huo aina ya jojo uliingizwa nchini toka mwaka juzi ukiwa umeharibika na ni hatari kuliwa kwa afya za binadamu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari wakati wa uteketezaji wa mchele huo, Mkurugenzi wa Maabara kutoka Mamlaka ya Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar, Nadir Khatib Hassan, alisema mchele huo uliingizwa nchini na mfanyabiashara mzalendo ukitokea Pakistan.

Kuteketezwa kwa mchele huo kumetokana na ziara Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman, aliyoifanya mwanzoni mwa wiki katika Bandari ya Malindi na kugundua makontena mawili mbili yaliyokuwa na mchele huo ulioingizwa na Suleiman Abdulla toka Machi, mwaka jana ukiwa umeharibika.

Nadir alisema mfanyabiashara huyo ametozwa faini ya Sh. milioni tatu kwa ajili ya kuteketeza mchele huo.

"Awali mfanyabiashara huyo alitakiwa kurejesha mchele huo alikoutoa au kulipa faini, lakini baada ya kutokuwapo na mawasiliano mazuri kati yake na kampuni aliyonunua mchele huo kutoka Parkistan, aliamua kulipa faini hiyo," alisema.

Alisema mchele huo kama ungetumika ungesababisha madhara mbalimbali ya kiafya kwa binadamu kwa sababu uliharibika sana baada ya kushambuliwa na wadudu.

Nadir alisema serikali haitokuwa tayari kuona wananchi wake wanaendelea kutumia bidhaa za vyakula zilizopitwa muda wake wa matumizi na kufanya hivyo ni njia ya kuwajengea mazingira mabovu ya afya zao.



Mfanyabiashara maarufu wa Zanzibar, Masoud Shalamaa, akielezea kero zinazowapata wageni (watalii) wanaotembelea Mjimkongwe, hasa uchafu na 'papasi' wanawasumbua wageni wanaotembelea mji huo na magari mengi kukosa sehemu ya kupaki na maeneo kadhaa kuhodhiwa na wenye hoteli. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

## Mwinyi apigia debe uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amewaomba wawekezaji kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kuwekeza nchini, hususan katika sekta ya utalii.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu Zanzibar, alipokuwa na mazungumzo na Balozi wa Falme za Kiarabu nchini Tanzania, Khalifa Abdulrahman Almarzouqi, aliyefika kujitambulisha.

Alisema katika dhana ya kuimarisha uchumi Zanzibar, inalenga kuimarisha uchumi wake kupitia uchumi wa bluu, hivyo inahitaji wawekezaji kutoka mataifa mbalimbali duniani, ikiwamo UAE ili kuwekeza kupitia sekta ya utalii yenye vivutio mbalimbali katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Serikali anayoiongoza, alisema inalenga kukifanya kisiwa cha Pemba kuwa eneo muhimu la uwekezaji, hivyo akawataka wawekezaji kutoka nchi hizo kufika kuwekeza katika miradi mbalimbali.

Alisema sheria za uwekezaji ikihusisha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya miradi mbalimbali, zinatoa fursa kwa wawekezaji kuwekeza katika maeneo mbalimbali yakiwamo ya visiwa.

Pia Dk. Mwinyi alitoa pongezi kwa nchi za jumuiya hiyo kwa uhusiano na ushirikiano mzuri na wa muda mrefu kati yake na Zanzibar, pamoja na misaada inayoendelea kutolewa kupitia nyanja za kiuchumi na kijamii.

Alisema nchi za Falme za Kiarabu zimekuwa zikiunga mkono juhudi za serikali, hivyo kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Zanzibar, ambapo kwa nyakati tofauti zimesaidia miradi kadhaa, ukiwamo mfuko wa 'Khalifa Fund' unaolenga kuwawezesha kiuchumi vijana wa Zanzibar.

Vilevile aliziomba taasisi na wadau wa maendeleo kutoka nchi hizo kuunga mkono juhudi za serikali zinazolenga kuuweka katika mazingira bora zaidi Mji Mkongwe wa Zanzibar (ulio katika urithi wa Ulimwengu) ili kuwa eneo la kiuchumi.

Naye Balozi Khalifa alisema UAE itaendeleza uhusiano na ushirikiano mzuri uliopo kati yake na Zanzibar, sambamba na kuendelea kuisaidia nchi hiyo katika nyanja za kiuchumi na kijamii.

Aidha, aliahidi kuwashajiisha wawekezaji wa nchi hizo kufika Zanzibar kuwekeza.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

**Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.**

## OFISI ZA MATANGAZO

Mikocheni Industial Area,
Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

## KUPOTEA KWA CHETI



**PRISCAR C. MWALUMPEMBE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1676-0008** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia MOMBA SEKONDARI mwaka 2017. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **IRI/IRI/RB/838865/2020.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**HIDAYA B.MSENGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina la **AMINA S.MHINA** aina ya **SANLG** yenye namba za usajili **MC 942 ARW.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/RB/6921/2020.**

**AMITIE ATTORNEYS COMPANY LIMITED**
**COMPANY NO. 139490**
**P.O BOX 1214,**
**MWANZA**

## NOTICE OF RESOLUTION TO WIND UP VOLUNTARILY

Pursuant to section 334(1) of the Companies Act, Cap 212 of 2002, we **AMITIE ATTONEYS COMPANY LIMITED** (hereinafter called "the Company") hereby give notice to the general public that on 01st day of November 2020 the shareholders of company resolved to wind up the company voluntarily pursuant to section 333(1)(1) of the Companies Act.

---

STEVEN EMMANUEL MAKWEGA
BOARD CHAIRPERSON /DIRECTOR

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**EMANUELI CHALILA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI YENYE NAMBA ZA **MC 219 CGS** AINA YA WANHOO. KWA YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH/TR/RB/MS/9138/2020**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA TEMEKE**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 152 YA 2020**

**MARIAM SALUM.................WADAI/MDAI**
**DHIDI YA**
**VERONICA PHILIP CHACHA.....MDAIWA/WADAIWA**

**KUITWA SHAURINI**
**VERONICA PHILIP CHACHA**

MARIAM SALUM amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Temeke (Usalama). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa/hukumu/maamuzi tarehe 21 mwezi 01 mwaka 2021 mbele ya Mhe. R. CHENYA. Hivyo basi mnatakiwa/unatakiwa kuleta utetezi wenu/wako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masjala ya wazi Baraza la Ardhi na Nyumba TEMEKE. Endapo hautatekeleza haya shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa. AMRI hii imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa Baraza hii leo tarehe 30 mwezi 12 mwaka 2020.

MWENYEKITI,
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA TEMEKE

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

**UZA, CHENYE THAMANI KUBWA KWA KUTANGAZA NASI**
**KWA BEI POA TUPIGIE MOB: +255 - 745 700 710**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Waandishi habari wasio na vibali waonywa kuripoti uchaguzi mkuu

**Kampala, UGANDA**

WAANDISHI wa habari, wasiokuwa na idhini ya kuripoti uchaguzi mkuu wa Uganda, wamezuiwa kufanya hivyo.

Inspekta Jenerali wa Polisi nchini humo, Meja Jenerali Paul Lokech, alitoa agizo hilo Jumatano usiku na kwamba limeanza kutekelezwa kuanzia, Desemba 31, mwaka jana.

Lokech alisema polisi wote na mashirika ya usalama yatawatambua wanahabari ambao wameidhinishwa na Baraza la Habari la Uganda kuripoti shughuli za kampeni na uchaguzi.

Taarifa yake imekuja baada ya kukamatwa kwa mabloga kadhaa na wachapishaji wengine wa mtandaoni.

Walikamatwa kwa kuhusishwa na Chama cha Upinzani cha National Unity Party ambao walikuwa wakiangazia kuzuiliwa kwa kampeni za Bobi Wine na kukamatwa kwa maofisa wa kampeni zake katika Wilaya ya Kati ya Kalangala.

Mwongozo mpya uliobuniwa hivi karibuni na Baraza la Habari, unawakata wanahabari nchini humo kando mbali na kulipa ada ya uanachama, kuwasilisha nakala za kazi zao na maelezo yao ya kibinafsi.

Wanahabari wa kigeni wanatakiwa kuwasilisha cheti cha uadilifu kutoka Shirika la Interpol.

Hata hivyo linaweza kukataliwa kwa misingi ya kutokuwa na maelezo ya kutosha, kutopata idhini ya vyombo vya usalama au kutoruhusiwa kukanyaga ardhi ya Uganda.

Hatua kali za uhakiki zilianzishwa muda mfupi baada ya serikali hivi karibuni, kuwafukuza wanahabari watatu wa Canada ambao walikuwa wameidhinishwa na Baraza la Habari kufanya kazi nchini humo.

Wiki mbili, kuelekea uchaguzi mkuu kuna ushindani mkali, huku serikali ikikosolewa kwa ukandamizaji wa uhuru wa vyombo vya habari na watetezi wa haki za binadamu.

Jenerali Lokech alisema agizo hilo jipya, litasaidia vyombo vya usalama kuwalinda waandishi wa habari.

Wakati huohuo, Kiongozi wa upinzani nchini humo, Bobi Wine amezuiwa tena kuhutubia wafuasi wake.

Siku ya Jumatano, alikamatwa na polisi, pamoja na wajumbe kadhaa wa timu yake wakati wakifanya kampeni katika wilaya ya kisiwa cha Bugala, Kaskazini mwa Ziwa Victoria.

Bobi Wine alikuwa ameanza tena kampeni yake ya urais nchini Uganda.

Mwanamuziki huyo ambaye kwa sasa ni mmoja wa wanasiasa wakuu wa upinzani na mkosoaji mkuu wa Rais Yoweri Museveni, alirejeshwa nyumbani kwake Magere, katika mji mkuu Kampala, chini ya ulinzi mkali wa polisi.

Polisi wa Uganda, wanalaumu mpinzani mkuu huyo wa Yoweri Museveni, kwa kukiuka sheria za kupambana na janga la covid-19 na kukanusha kuwa wamemkamata.

"Mgombea huyo alishikiliwa kwa kuendelea kuandaa mikutano mikubwa wakati nchi inakabiliwa na tishio la janga la COVID-19, kwa kupuuza maagizo ya Tume ya Uchaguzi na Wizara ya Afya," polisi ilisema.

Tukio hilo lilitokea katika Wilaya ya Kalangala, kwenye Kisiwa cha Bugala Kaskazini mwa Ziwa Victoria.

"Hii sio moja ya maeneo ambayo kampeni imepigwa marufuku kwa sababu ya corona. Hili eneo ilikuwa kwenye ajenda ya mzunguko wa kampeni yetu, "alisema msemaji wa chama cha Bobi Wine, Joel Ssenyonyi.

Bobi Wine, ni mshindani mkali wa Rais Yoweri Museveni mwenye umri wa miaka 76, kuelekea uchaguzi mkuu wa Januari 14, mwaka huu.

***BBC/RFI***




Gari likiwa limeharibiwa vibaya baada ya tetemeko kupita katika eneo la Sisak, nchini Croatia, jana. **PICHA/REUTERS**

# Wahamiaji 500 waachwa bila makazi

**Konjic, BOSNIA**

WAHAMIAJI 500 na wakimbizi wameachwa bila makazi nchini Bosnia, jana, baada ya maandamano ya wenyeji kulizuia basi kuwapeleka katika vituo vingine vya kuwahifadhi.

Wahamiaji hao, ambao wamekuwa wakilala kwenye baridi tangu kambi ya Lipa ilipovunjwa na Shirika la Kimataifa la Wahamiaji (IOM), Desemba 23, mwaka jana, walitarajiwa kupelekwa makazi mengine ya mji wa kati wa Konjic Jumanne.

Hata hivyo, baada ya maandamano ya wakazi wa mji huo, mabasi hayo yaliondoka bila kuwabeba wahamiaji hao jana mchana.

Kundi hilo liliachwa mitaani lijitegemee kivyake.

Inaripotiwa kuwa serikali ya Bosnia, imewapa kambi ya zamani ya kijeshi katika wilaya ya Bradina kama makazi yao mapya.

***DW***

# 28 wafariki dunia shambulio Syria

**Damascus, SYRIA**

RAIA 28 wameripotiwa kupoteza maisha na wengine 13 kujeruhiwa, kwenye shambulizi lililotekelezwa katika basi la usafiri nchini Syria.

Kulingana na taarifa za Shirika la Habari la Serikali ya Syria (SANA), iliarifiwa kwamba basi lililokuwa limebeba raia lilishambuliwa katika eneo la Kebacib, lililoko barabara kuu ya Deyrezzor-Tedmur, jana, saa 10 jioni.

Taarifa zaidi zilisema kufariki kwa raia 28 na kujeruhiwa kwa wengine 13, kulitokana na shambulizi hilo.

Kundi la silaha lililoendesha shambulizi hilo lilitokea upande wa Mkoa wa Tanf, ambao uko chini ya udhibiti wa vikosi vya Marekani, karibu na mpaka wa Jordan, ambapo baadaye walitoweka jangwani baada ya kuteketeza basi.

***TRT***

# Dola 150,000 kuzifidia familia ajali ya ndege Ukraine

**Tehrana, IRAN**

IRAN imeidhinisha malipo ya fidia kwa familia za watu waliouawa kwenye ndege iliyolengwa kwa bahati mbaya.

Imeamua kulipa fidia ya dola 150,000 kwa familia za kila mtu aliyepoteza maisha katika ndege ya abiria ya Shirika la Ndege la Ukraine, ambayo iliangushwa na kombora kwa bahati mbaya mnamo Januari, mwaka jana.

Fidia inayolipwa kwa familia za waliopoteza maisha kwenye ndege hiyo, iliidhinishwa na Baraza la Mawaziri. Baraza la Mawaziri, liliidhinisha malipo ya dola 150,0000 kwa familia na jamaa za kila mmoja ya wale waliokufa kwenye ndege ya Ukraine haraka iwezekanavyo.

Ndege ya abiria ya aina ya Boeing 737 ya Ukraine, iliangushwa muda mfupi baada ya kuruka kutoka uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Imam, Khomeini mjini Tehran kwenda Kiev, Januari 8, mwaka jana. Kwenye ajali hiyo hakunusurika abiria yeyote kati ya 176 aliyekuwamo katika ndege hiyo.

Hapo awali, maofisa wa Iran walikuwa wakikanusha madai ya kuilenga ndege hiyo na baadaye Idara ya Ulinzi ikatangaza kwamba, ndege hiyo ya Ukraine ilipigwa kombora kwa bahati mbaya baada ya makombora mawili yaliyorushwa na mfumo.

Saa chache kabla ya kuangushwa kwa ndege hiyo, Jeshi la Ulinzi wa Mapinduzi ya Iran, lilifanya shambulizi la kombora kwenye kambi za Marekani, zilizoko nchini Iraq, kulipiza kisasi cha mauaji ya Jenerali wa Iran, Qassem Soleimani.

***DW***




# ZIDANE:

## HAZARD ANAHITAJI MUDA KUWA BORA

**MADRID, Hispania**

KOCHA Mkuu wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amesema, Eden Hazard anahitaji muda zaidi ili kurudi katika ubora wake na kuanza, baada ya kupona majeruhi na kuchezeshwa kwenye mchezo wa Jumatano wa sare dhidi ya Elche.

Hazard aliingia akitokea benchi kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Madrid wakati wakitoka sare ya kufungana 1-1 na Elche, akiwa hajaichezea Los Blancos hao tangu Novemba, mwaka 2020.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji, ambaye alikuwa benchi na hakutumika kwenye mchezo wa mwishoni mwa wiki iliyopita dhidi ya Granada, aliingizwa uwanjani zikiwa zimebakia dakika 13 mpira kumalizika.

"(Eden Hazard) anahitaji muda, anahitaji muda wa kucheza zaidi na pole pole kwa uhakika kabisa atarudi kwenye kikosi cha kwanza," alisema Zidane akiwaambia waandishi wa habari.

"Sidhani kama tulitakiwa kufunga bao la pili katika kipindi cha kwanza, kwa sababu tulicheza vizuri dhidi ya Elche na tulikuwa na wakati mgumu kipindi cha pili, lakini tunatakiwa kuendelea kujituma na kuimarika zaidi, kwa sababu kuna mechi nyingi bado za kucheza kwenye LaLiga."

Madrid ilishindwa kuwapiku vinara Atletico Madrid baada ya kushinda kwao mechi tano mfululizo kwenye ligi hiyo kufikia mwisho Jumatano.

Luka Modric aliiweka mbele kwa kufunga bao dakika ya 20 kwa kichwa, kabla ya penalti ya Fidel dakika saba baadaye kusawazisha bao hilo.

Miamba hao wa Hispania, Madrid wamegonga mwamba mara 18 katika mashindano yote msimu huu, mara nyingi zaidi kuliko timu yoyote katika ligi kubwa tano kubwa Ulaya.

Madrid imepitwa pointi mbili na Atletico ambao wana mechi mbili mkononi na Zidane aliongeza: "Kama ukiangalia mambo yalivyokwenda tulipokuwa tukicheza katika siku za hivi karibuni, sare hii inawezekana kuwa siyo matokeo mazuri."

# AC MILAN WAAMULIWA KUMLIPA BOBAN

**MILAN, Italia**

AC Milan imeshindwa kesi dhidi ya aliyekuwa Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo, Zvonimir Boban, kwa mujibu wa Sky Sport.

Katika kesi iliyofunguliwa na Boban dhidi ya klabu yake hiyo ya zamani alishinda na mahakama ya jiji la Milan iliiamuru alipwe euro milioni 5.3 kama fidia.

Boban alitumbuliwa Machi, mwaka jana, lakini kulikuwa na mshike mshike kwenye sababu ya kutimuliwa kwake na mkurugenzi huyo wa zamani akaamua kufungua kesi dhidi ya klabu yake hiyo aliyoichezea kwa mafanikio makubwa.

Sababu kubwa ya kufukuzwa kwake ilitajwa kuwa ni kumtuhumu Mkurugenzi Mkuu, Ivan Gazidis, kufanya mambo nyuma ya mgongo wake, akimaanisha hakuwa anashirikishwa ipasavyo kwa baadhi ya mambo nyeti.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka nchini Italia, zilibainisha Boban ameshinda kesi hiyo, na anatarajia kulipwa faini kama ilivyoamriwa na mahakama.

Hata hivyo, msimamo wa Milan ni kwamba, wao walikamilisha kila kitu kama inavyohitajika na wanatarajia kukata rufani dhidi ya uamuzi huo.

Kupitia taarifa ya AC Milan, wameweka wazi nia yao ya kukata rufani dhidi ya uamuzi huo.



# BALOTELLI AANZA KWA BAO MONZA

**ROME, Italia**

MARIO Balotelli alianza maisha yake kwa mara ya kwanza kwenye Ligi ya Serie B, kwa kufunga bao dakika tatu tu baada ya kuanza kuichezea Monza dhidi ya Salernitana.

Mchezaji huyo wa zamani wa Milan na Manchester City, Balotelli alisajiliwa na Monza, inayomilikiwa na mmiliki wa zamani wa Milan na Waziri Mkuu wa zamani wa Italia, Silvio Berlusconi, mapema Desemba mwaka jana hadi mwisho wa msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, alicheza kwenye mchezo huo uliopigwa Jumatano pamoja na Kevin-Prince Boateng, nyota mwingine aliyecheza nae kule Milan kwa vinara hao wa Serie B.

Na Balotelli alihitaji dakika tatu na sekunde 53 kufunga bao akiunganisha krosi ya Carlos Augusto likiwa shuti lake la kwanza na akigusa mpira kwa mara ya kwanza.

Balotelli alizichezea timu kubwa za Ligi Kuu Italia, Serie A, England na Ufaransa akiwa na Nice mwaka 2016, ambako pia alifunga kwenye mchezo wake wa kwanza.





# KLOPP

## AFURAHIA THIAGO KURUDI DIMBANI

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amebainisha namna alivyosubiri kwa muda mrefu kurudi dimbani kwa kiungo, Thiago Alcantara.

Thiago alitokea benchi na kuingia kwenye mchezo wake wa kwanza tangu Oktoba, mwaka jana, wakati Liverpool ikitoka suluhu na Newcastle United kwenye mchezo wa Ligi Kuu England uliochezwa juzi Jumatano.

Nyota huyo wa zamani wa Bayern Munich, ambaye aliumia goti wakati wakitoka sare ya 2-2 dhidi ya Everton, Oktoba 17, mwaka jana, aliingia dakika ya 73 na akapiga pasi 23 huku asilimia 91.3 zikiwa za uhakika.

"Tulimsajili Thiago kwa sababu tulifikiria ni mchezaji mzuri, hivyo unaweza kufikiria namna unavyotaka kumwona kwenye timu. Huo ndio ukweli," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Kile kilichofanywa na vijana wengine wakati yeye akiwa hayupo dimbani kwa uhakika kabisa kilikuwa cha aina yake.


"James Milner, kwa mfano, usiku huu (juzi) alicheza mchezo wa aina yake kwenye safu ya kiungo.

"Kwa uhakika. Hivyo, yeye ni mchezaji mzuri na amerudi, ni mchezaji wa kiwango cha juu. Nafikiri katika dakika zake 20 za mwanzo, zilikuwa bora zaidi.

"Alifanya mazoezi mara mbili tu na timu. Bado kimwili hajawa fiti sana, naamini kuna mengi zaidi yanakuja kutoka kwake."

Sare hiyo imewafanya Liverpool sasa kuongoza msimamo wa Ligi Kuu England kwa tofauti ya pointi tatu dhidi ya Manchester United waliopo nafasi ya pili.

## ARTETA: MIPANGO YA USAJILI HAIJABADILIKA



**LONDON, England**

BAADA ya kupata ushindi wa mechi mbili mfululizo, kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, amesema bado malengo yake hayatabadilika katika dirisha dogo la usajili la Januari.

Ubora waliouonyesha vijana kama Bukayo Saka na matokeo yaliyopatikana katika mechi mbili zilizopita hazitabadili chochote.

Arsenal hawakupata ushindi katika mechi saba wakiwa katika nafasi ya 15 katika jedwali wakati wa Chrismasi, lakini kutoka hapo wamefanikiwa kuwafunga Chelsea na Brighton and Hove Albion.

Ushindi wa 1-0 dhidi ya Brighton, kwa bao lililofungwa na Alexander Lacazette akitokea benchi siku ya Jumanne uliwapa alama tatu muhimu.

"Hapana, matokeo ya mechi hizi mbili hayatabadili mipango yetu kuelekea dirisha la usajili," alijibu Arteta alipoulizwa na waandishi wa habari kama matokeo hayo yana maana yoyote kuelekea dirisha la usajili la Januari.

"Tulipanga kuingia sokoni, hivyo hadi sasa hakuna kilichobadilika, lazima tuingie sokoni kwa ajili ya kuimarisha kikosi chetu."



## INTER YAKARIBIA KUMNASA GOMEZ

**MILAN, Italia**

INTER Milan inakaribia kumsajili nyota wa Atalanta, Papu Gomez, huku ripoti zikisema kwamba, wameshafikia makubaliano binafsi ya awali na mchezaji huyo.

Gomez anafanya mazoezi binafsi tofauti na wachezaji wenzake, hata baada ya mapumziko ya Krismasi na anatarajiwa ataendelea kufanya mazoezi kwa kujitenga baada ya kutokuwa na maelewano na kocha, Gian Piero Gasperini.

Wakati Milan, Roma, Napoli na klabu kadhaa za Ligi Kuu Marekani, MLS, zikiwa zinavutiwa na saini ya nyota huyu, Inter bado ndio wenye nafasi kubwa zaidi.

Kwa mujibu wa gazeti la Corriere dello Sport, Inter wanamtaka kwa bei sahihi, ambayo ni bei ya chini kuliko bei ya awali ya euro milioni 15.

FCInterNews pia wameripoti kwamba, Gomez ameshughulikia masharti ya awali na Inter, kwa mkataba unaoweza kumweka hadi Juni, mwaka 2023 wenye thamani ya euro milioni 2.5 kwa msimu pamoja na bonasi.

Fedha za usajili huo kwa Inter, zinaweza kupatikana kwa kumuuza Andrea Pinamonti, wakati mchezaji wa timu ya vijana, Gaetano Oristano pia anaweza kujumuishwa katika dili hilo.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO KUCHEZA SOKA HADI UZEENI

●●●Nahodha huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno afunguka kwake umri mkubwa si tatizo...

**TURIN, Italia**

CRISTIANO Ronaldo amesisitiza ndoto yake ni kucheza kwa miaka mingi kadri iwezekanavyo na kushinda Kombe la Dunia.

Nyota huyo wa Juventus ambaye ameshinda Ballon d'Or mara tano, anaongoza kwa mabao katika Ligi Kuu Italia -Serie A, licha ya timu yake kuwa nafasi ya sita na kutofautiana kwa pointi 10 na vinara AC Milan.

Ronaldo hadi sasa anahitaji mabao saba tu ya kwenye mechi za kimataifa ili aweze kuifikia rekodi ya dunia ya Ali Daei (kutoka Iran) ya mabao 109.

"Suala la umri halijalishi. Kinachohitajika ni akili. Haijalishi kama Cristiano Ronaldo ni bora, huwezi jua nini kitatokea," alisema Ronaldo akinukuliwa na Sky Sport Italia.

"Ninaishi sasa, wakati huu. Wakati huu ni mzuri, ninahisi furaha na ninajiona niko vizuri katika wakati mzuri wa maisha yangu. Ninatumaini nitacheza miaka mingi, mingi zaidi lakini hauwezi kujua."

Ronaldo alianza kucheza soka la kulipwa akiwa na Sporting Lisbon, ambako alicheza mechi 31 tu kati ya mwaka 2002 na 2003, kabla ya kuondoka kwenda Manchester United wakati huo akiwa na umri wa miaka 18.

Baada ya miaka sita na United, akiwa amecheza mechi 292 alihamia Real Madrid mwaka 2009, ambako alisalia akisakata kabumbu hadi mwaka 2018 alipoamua kuhamia Juventus.

Nyota huyu anaamini ndoto yake inawezekana licha ya kutambua uhalisia kuwa 'hakuna ajuaye kesho' hivyo chochote kinaweza kutokea, lakini ana matumaini makubwa katika kutimiza ndoto yake.

## KWA UFUPI

**MESSI KUONDOKA 2023**

NYOTA wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, huenda akabakia Barcelona hadi mwaka 2023, kabla ya kujiunga na klabu ya David Beckham, Inter Miami. Messi amenunua nyumba yenye thamani ya pauni milioni 7.25 mjini Miami na kwamba anadaiwa kutaka watoto wake kujiunga na shule Marekani. ***(Cadena, via Mail)***

**AARONS ANUKIA UNITED**

MANCHESTER United imeimarisha nia yake ya kutaka kumsajili mlinzi wa Norwich, Max Aarons mwenye umri wa miaka 20, lakini watalazimika kusubiri hadi msimu ujao kwa kumchukua mchezaji huyo wa Timu ya Taifa ya England ya umri chini ya miaka 21. ***(Sun)***

**WIJNALDUM SOKONI**

KLABU ya Wolves imejiunga kwenye mbio za kuwania kumsajili kiungo wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Georginio Wijnaldum, mwenye umri wa miaka 30. ***(Gazzetta dello Sport, via Mirror)***

**HAALAND ATAJWA BARCA**

MGOMBEA wa urais katika klabu ya Barcelona, Emili Rousaud, amesema atamsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20, kama atachaguliwa kuwa rais wa Barca. ***(Marca)***

**ISCO AITAKA CHELSEA**

MCHEZAJI anayewindwa na Arsenal, Isco, amekiri kwamba angependa kuichezea klabu ya jijini, London, Chelsea. ***(Mirror)***

**CHELSEA YAMTAJA SANCHO**

CHELSEA inatarajiwa kujiunga na Manchester United na Liverpool katika mbio za kuwania saini ya winga wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20. ***(Que Golazo, via Football London)***

**FASU-MENSAH AGOMA**

MLINZI wa Manchester United na Uholanzi, Timothy Fosu-Mensah mwenye umri wa miaka 22, amekataa ofa ya mkataba mpya wa miaka mitatu na nusu. ***(Mirror)***

**MARSEILLE, HERTHA VITANI**

KLABU za Marseille na Hertha Berlin zipo kwenye mbio ya kuwania saini ya mlinzi wa Manchester United, Timothy Fosu-Mensah mwenye umri wa miaka 22 wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari hii. ***(Sky Sports)***

**BROAAF ANUKIA DORTMUND**

BORUSSIA Dortmund inawania kumsajili kinda aliyepo kwenye akademi ya Manchester City, Jayden Braaf, raia wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 18, ambaye huenda akaruhusiwa kuondoka Januari hii. ***(Bild, via Manchester Evening News)***

**KOLASINAC KUREJEA SCHALKE**

MLINZI wa kushoto wa Arsenal na Bosnia and Herzegovina, Sead Kolasinac mwenye umri wa miaka 27, yupo kwenye majadiliano na klabu yake ya zamani wa Schalke ili kwenda kucheza kwa mkopo. ***(Mail)***

**JUVE YAMFUATA LLORENTE**

JUVENTUS inawania kumsajili straika mkongwe wa Hispania, Fernando Llorente. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 kwa sasa anacheza katika klabu ya Napoli. ***(Tuttosport)***

**TREZEGUET ANUKIA UTURUKI**

MIAMBA ya Uturuki, Galatasaray inataka kumsajili wa mkopo kiungo wa Aston Villa na Misri, Trezeguet mwenye umri wa miaka 26, wakati wa dirisha dogo la Januari hii. ***(Vatan, via AS)***

HABARI MICHEZO

# MAHADHI 'MOYO' YANGA, MWILI UMESIMAMA IHEFU

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa Ihefu ya jijini Mbeya, Juma Mahadhi, amesema anaamini atafanya vyema katika klabu yake hiyo anayoitumikia kwa mkopo, ili ajitengenezee mazingira ya mazuri ya kurejea tena Yanga katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mahadhi ambaye anaichezea Ihefu kwa mkopo baada ya kutua katika kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili, tayari amesh-acheza mechi kadhaa zikiwamo mbili dhidi ya timu yake 'mama' ya Yanga, amesema kuwa hayuko tayari kujitathmini mwenyewe ila amewaachia wadau wanaomwangalia anapokuwa uwanjani kuzungumzia kiwango chake.

Kiungo huyo alisema licha ya timu yake kufungwa mabao 4-0 na Simba, bado anaiheshimu kwa sababu ya kumpa nafasi ya kuonyesha kipaji chake kwa mara nyingine.

"Nataka nicheze, watu ndiyo wataona kiwango changu, hapa ndipo nitaonyesha kwa sababu tangu nipone majeraha yangu, sijapata hata dakika mbili za kucheza ndani ya Yanga, lakini huku baada ya kufika tu kila mtu kaona mechi zote zimecheza. Naamini sidhani kama nikifanya vizuri Yanga washindwe kunirudisha," alisema Mahadhi.

Kuhusu kupoteza mechi dhidi ya Simba, alisema Simba waliwazidi mbinu, lakini anaamini kuwa Ihefu itafanya vyema kwenye mechi za mzunguko wa pili ingawa bado hawajapata muunganiko kutokana na kuchezesha wachezaji wengi waliosajiliwa kipindi hiki cha dirisha dogo.

"Muunganiko bado. Wachezaji wengi tunaocheza ni wale tulioingia wapya. Tumecheza na Simba na Yanga, hizi ni timu kubwa, lakini zilizobaki ni saizi yetu tu, tutapambana nazo," Mahadhi alisema.

Kiungo huyo alijiunga na Yanga mwaka 2016 akitokea Coastal Union ya jijini Tanga.




Kiungo wa mabingwa watetezi, Simba, Luis Miquissone (kushoto), akijipanga kuwatoka wachezaji wa Ihefu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam juzi. Simba ilishinda mabao 4-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mapinduzi Cup mambo yameiva

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KATIKA kuonyesha kipute cha mashindano ya Kombe la Mapinduzi kimekaribia, Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo wa Zanzibar, Tabia Maulid Mwita, amepokea zawadi zitakazotolewa kwa washindi katika michuano hiyo kwa upande wa wanawake na wanaume, imefahamika.

Zawadi hizo za washindi zilitolewa jana na mfanyabiashara maarufu visiwani hapa na ambaye aliwahi kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, Mohamed Raza.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhiwa zawadi hizo, Waziri Tabia alisema mchango aliotoa mfanyabiashara huyo ni wa kuigwa na wafanyabiashara wengine wa Zanzibar, ili kufufua michezo na kuifanya kuwa na hadhi kubwa kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Waziri huyo alisema mchango huo alioutoa utaweza kusaidia moja kwa moja katika kufanikisha mashindano hayo ambayo yanatarajia kufanyika kuanzia Januari 5, mwaka huu.

Kiongozi huyo pia alimwomba Raza kuwashawishi wafanyabiashara wenzake kuwekeza katika sekta ya michezo ili kwenda na kasi ya Rais wa Zanzibar ya kutaka michezo iwe chanzo cha kutoa ajira nyingi kama zilivyo kwa nchi nyingine zilizoendelea.

Naye Raza alisema anamwahidi waziri huyo kuwa ataendelea kushirikiana na serikali katika kuhakikisha michezo inarudi katika hadhi yake.

Hata hivyo Raza aliita Wizara ya Michezo kwa kushirikiana serikali kuangalia uwezekano wa kurejesha mashindano ya Kombe la Muungano kwa lengo la kuliweka soka la Zanzibar katika ramani.

Zawadi alizokabidhi mfanyabiashara huyo ni vikombe vitatu kwa washindi wa Kombe la Mapinduzi kwa Wanaume, vikombe vitatu kwa washindi wanawake, medali, na zawadi nyingine ambazo kamati ya mashindano itazitoa pamoja na maji katoni 100 maalumu kwa timu za wanawake zinazoshiriki mashindano hayo.

## Chama amvuruga nahodha Ihefu FC

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA wa Ihefu FC, Joseph Kinyozi, ameeleza kufurahishwa na kiwango kikubwa kilichoonyeshwa na kiungo wa Simba, Clatous Chama na kusema wachezaji wa Tanzania wanatakiwa kujifunza mbinu kutoka kwa Mzambia huyo.

Akizungumza baada ya timu yake kuchapwa mabao 4-0 na Simba katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara juzi, Kinyozi alisema Chama ndiye mchezaji aliyemvutia zaidi kwenye mechi hiyo, lakini ni nyota ambaye ana uwezo mzuri wa kutandaza soka kwa kiwango cha juu kwenye ligi hiyo.

"Mimi nimeona mchezaji aliyenifurahisha leo ni Chama. Na siyo leo tu, huyu jamaa anajua bwana. Mimi nampenda sana huyu jamaa anavyocheza na kuna vitu naiga kutoka kwake. Mimi nasema hivi jamaa anajua na namwambia sisi wachezaji wa Tanzania tunampenda kwa sababu anachofanya kinatupendezesha," Kinyozi alisema. Kinyozi ambaye ni straika tegemeo wa Ihefu mwenye mabao matatu mpaka sasa, alisema mbinu kadhaa ambazo ameziiga kutoka kwa Chama zimekuwa zikimsaidia katika baadhi ya mechi anazocheza zikiwamo za Ligi Kuu.

"Kiukweli mimi namwambia kuwa kipaji hicho alichojaaliwa na Mwenyezi Mungu akiendeleze, azidishe juhudi kwa sababu yeye anaweza," aliongeza nahodha huyo. Kuhusu kubugizwa idadi hiyo ya mabao, Kinyozi alisema walifanya makosa kadhaa na kwa sababu walicheza na timu kubwa na ngumu, wameadhibiwa kutokana na upungufu huo.

## KMC yaitambia Mbeya City FC

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la KMC FC limesema limejiimarisha kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mbeya City kwa ajili ya kuondoka na pointi tatu katika mchezo huo, imeelezwa.

Mbeya City inatarajia kuwakaribisha KMC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Sokoine jijini, Mbeya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KMC, Habibu Kondo, alisema walifika salama Mbeya na morali ya wachezaji wake iko juu.

Kondo alisema wamekwenda Mbeya kwa kazi moja ya kusaka ushindi na hivyo kila mchezaji ameahidi kuonyesha kiwango kizuri katika mchezo huo.

"Tunashukuru tulifika Mbeya salama, lengo ni kuondoka na pointi tatu katika mchezo huu, tunajua wenyeji wetu pia wanazihitaji pointi hizo, lakini tunasema wasahau kuzipata kutoka kwetu," alisema Kondo.

Kocha huyo alisema anaupa umuhimu mchezo huo kwa kufahamu msimu huu kila timu imejipanga vizuri kupata pointi tatu katika kila mchezo.

Alisema licha ya kuwa ugenini watahakikisha wanatimiza ahadi ya kurudi na ushindi nyumbani na kuomba mashabiki waendelee kuwapa sapoti.

Michezo
Ijumaa Januari 1, 2021
Nipashe



RONALDO KUCHEZA SOKA HADI UZEENI HABARI UK 22



Winga wa Yanga, Tuisila Kisinda (kushoto), akijiandaa kupiga mpira dhidi ya beki wa Tanzania Prisons, Benjamin Asukile katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga mkoani Rukwa jana. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# NTIBAZONKIZA AIOKOA YANGA

## ●●●Ni kwa bao lake la kusawazisha dhidi ya Prisons, yaendelea kushikilia rekodi...

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI aliyesajiliwa katika dirisha dogo la usajili, Saido Ntibazonkiza amefanikiwa kuiokoa Yanga kwa kufunga bao la kusawazisha dhidi ya Tanzania Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyomalizika kwa sare ya goli 1-1 iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela Mjini Sumbawanga jana.

Ntibazonkiza alifunga bao hilo dakika ya 76, na kuiokoa Yanga na kipigo, hivyo kuifanya timu pekee ambayo mpaka sasa haijapoteza mchezo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu unaoendelea.

Ilikuwa ni mechi kali, iliyokuwa na matumizi makubwa ya nguvu, huku wachezaji wakishindwa kumudu kucheza pasi nyingi kutokana na uwanja kuwa na madimbwi ya maji, yaliyochanganyika na matope.

Hii ilitokana na mvua kubwa iliyonyesha Sumbawanga na kuufanya Uwanja wa Nelson Mandela kuwa si rafiki kwa wachezaji ambao walilazimika kupiga mipira mirefu.

Kwa matokeo hayo, timu hizo zimeshindwa kufungana msimu huu, kwani kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa Septemba 6, mwaka jana, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, timu hizo pia zilitoka sare ya bao 1-1.

Dakika ya pili tu, ilitokea sekeseke kwenye lango la Prisons, iliyotokana na mpira kutuama kwenye kidimbwi cha maji, lakini mabeki wa timu hiyo walifanikiwa kuondoa hatari hiyo huku dakika ya 21, nusura Prisons ijipatie bao baada ya faulo iliyopigwa na Jeremiah Juma, lakini kipa Metacha Mnata aliuchupia na kuupangua.

Krosi iliyopigwa na Lambart Subianka, nusura itinge wavuni yenyewe dakika ya 24, lakini mpira ukapita juu kidogo ya lango la Yanga na kuwanyima wenyeji nafasi nyingine ya kufunga bao katika mchezo huo.

Prisons ingeweza tena kujipatia bao dakika ya 30 baada ya nahodha wake, Benjamin Asukile akiwa mita 30 hivi, aliachia shuti kali lililotoka nje kidogo ya lango, huku Metacha akiwa ameshakubali matokeo.

Dakika moja baadaye Salum Kimenya, akiwa ndani ya eneo la hatari alipiga shuti ambalo lilipanguliwa na Metacha, kabla ya kuokolewa na mabeki wa Yanga wakati Yassin Mustapha, aliyeambaa na mpira wingi ya kushoto na kuachia shuti kali lililompita kipa Jeremiah, lakini ukatoka nje kidogo ya lango la Prisons. Kipindi cha pili ndicho kilichoonekana kuchangamka zaidi kwa dakika sita tu baada ya kipindi hicho, kiungo mkabaji, Jumanne El Fadhili, aliipatia Prisons bao akiunganisha faulo iliyopigwa na Kimenya.

Baada ya Yanga kusawazisha, ilionekana kucharuka na kufanya mashambulizi mengi langoni mwa Prisons, lakini mabeki wa timu hiyo, wakiongozwa na Ismail Mhesa, Asukile, Vedatus Mwihambi na Nurdin Chona walisimama imara kuokoa hatari zote kutoka kwa Michael Sarpong, Tuisila Kisinda, Ntibazonkiza na wengineo.

Sare hiyo inahitimisha ushindi wa mechi sita mfululizo ambao Yanga iliopata, tangu ilipotoka sare ya bao 1-1 Novemba 22, mwaka jana dhidi ya Namungo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Mechi ilizoshinda ni dhidi ya Azam FC, JKT Tanzania, Ruvu Shooting, Mwadui, Dodoma Jiji, na Ihefu FC.

Kwa matokeo hayo, Yanga inaendelea kuongoza kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa imefikisha pointi 44, ikicheza mechi 18, huku Prisons ikiwa kwenye nafasi ya tisa baada ya kufikisha pointi 22.

Azam leo imezinduka kwa kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania wakati Coastal Union iliyokuwa nyumbani kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani imelazimishwa sare ya bao 1-1 na Namungo FC kutoka mkoani Lindi.

## SIMBA YATARAJIA MAKUBWA 2021

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kufunga mwaka na ushindi mnono wa mabao 4-0 dhidi ya Ihefu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema wanajiandaa kufanya vizuri zaidi kwenye mwaka mpya na wataanza kwa kupata ushindi mzuri watakapowakaribisha FC Platinum kutoka Zimbabwe.

Simba inatarajia kuwakaribisha FC Platinum katika mchezo wa marudiano wa hatua ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa Januari 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Sven alisema ni ushindi walioupata juzi ulikuwa ni muhimu kwao kwa kumaliza mwaka 2020 vizuri na sasa wanaelekeza nguvu ya kuanza kwa kishindi mwaka 2021 kwa kuwaondoa FC Platinum.

Sven alisema Ihefu hawakuwa vizuri katika kipindi cha kwanza ambacho timu yake ilifunga mabao matatu, lakini walibadilika kipindi kilichofuata na kuwapa Simba mazoezi mazuri kuelekea mchezo wao wa kimataifa.

"Kuhusu kiwango cha Said Ndemla, amefanya majukumu yake vizuri na unapopata ushindi wa mabao 4-0 sio wa mchezaji mmoja, ni juhudi za wachezaji wote. Huu ni ushindi mzuri kwa kufungia mwaka, tusahau matokeo hayo tunaenda mapumziko ya siku mbili tukirejea uwanjani, tunaendelea na maandalizi dhidi ya FC Platinum," alisema Sven.

Kocha huyo alieleza wanatarajia kukutana na mchezo wenye ushindani kwa sababu wanahitaji kupata matokeo mazuri, ili wasonge mbele katika mashindano hayo.

"Mechi ya kwanza tulipoteza tukiwa ugenini, nadhani hatukustahili kupoteza kwa sababu tulicheza mpira nzuri, sasa tupo nyumbani tunahitaji kupambana kutafuta matokeo mazuri katika mechi hiyo inayotoa uamuzi wa nafasi yetu," alisema Sven.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema hatima ya kiungo wao, Jonas Mkude aliyesimamishwa itajulikana wiki ijayo baada ya Kamati ya Nidhamu ya klabu hiyo kukutana na kumjadili nyota huyo.

"Mashabiki wasiwe na wasiwasi Kamati ya Nidhamu itafanya kazi yake, hakuna sehemu ya kazi watafurahishwa na kufumbia macho mfanyakazi asiye na nidhamu," alisema Barbara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002